




UKURASA 3

## ADAIWA kumuua baba kushindwa kumtafutia mke


Nipashe TESA
Jumanne Septemba 6, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Wahadzabe 'wafalme wa msituni' waliobobea kulinda kila kiumbe
Una maoni kuhusu ubunifu, teknolojia?
ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA
Aliyetibuliwa mpango wa kuozwa asimulia mwanzo, mwisho mambo yalivyokuwa
•Wazazi mkoa anakotoka waaswa 'tafakarini njia zenu'

UKURASA 11

# Nipashe

Jumanne Septemba 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581060

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Bei ya nafaka yazidi kupanda

**WANANCHI** waelezea machungu wanayopitia ... *Endelea uk. 2*




Baadhi ya bei za bidhaa zilizouzwa maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Samia apanda boti Zanzibar hadi Dar, alipa nauli kamili

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasalimia abiria aliosafiri nao kwa meli ya M.V Kilimanjaro 4 katika Bandari ya Malindi Zanzibar kwenda jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## MWINYI AKERWA WIZI WA MABILIONI SERIKALINI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameonesha kukerwa na wizi wa mabilioni ya fedha katika serikali na kuahidi kuteua Mkurugenzi Mkuu mpya wa Mamlaka ya Kuzuia...

## Raila Odinga akubali yaishe

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA NA KISINDA SASA KIMEUMANA** UK.24 **KABWELA** UK. 18



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akiwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kigali nchini Rwanda, ambapo anatarajia kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Mapinduzi ya Kijani Barani Afrika wa Mwaka 2022 (AGRF 2022), unaofanyika nchini humo kuanzia leo hadi Septemba 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bei ya nafaka yazidi kupanda

**Na Jenifer Gilla**

BEI ya bidhaa za nafaka imeendelea kupanda hali inayowafanya baadhi ya wananchi kupata milo miwili kwa siku ili kukabiliana na hali hiyo.

Nipashe ilitembelea maeneo mbalimbali ya Dar es Salam na kubaini kupanda bei za bidhaa zinazotumiwa na kwa mlo wa kila siku ambazo ni mchele, maharagwe, unga wa ngano, unga wa sembe, dona na choroko.

Mchele kilo moja umepanda kutoka Sh. 1,800 au 2,000 hadi Sh. 2,700 daraja la kwanza na super kutoka Sh. 2,500 hadi 3,500, unga wa sembe na dona umetoka Sh. 1,200 hadi Sh. 1,600 na unga wa ngano Sh. 1,300 hadi 2,000 kwa kilo huku choroko ikipanda kutoka Sh. 1,500 hadi Sh. 2,500. Bei ya mfuko wa kilo tano za unga imepanda kutoka Sh. 6,000 hadi 8,000.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wamesema kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa hizo, wamelazimika kula milo miwili kwa siku badala ya mitatu.

Mkazi wa Tabata, James Macha, alisema analazimika kutokunywa chai ya asubuhi kutokana na kupanda kwa bei za vitafunwa ikiwamo chapati, maandazi na vitumbua, hivyo ili aweze kumudu gharama nyingine za maisha ikiwamo kulipa kodi ya nyumba na kulipa ada ya shule.

Macha, mwenye mke na watoto wawili, alisema kabla ya kuchukua uamuzi huo, sasa anatumia Sh. 3,000 kwa ajili ya kununua vitafunwa asubuhi kutoka Sh. 1,200 aliyokuwa anatumia awali. Alisema hali hiyo imetokana na vitafunwa hivyo kupunguzwa kipimo, hivyo kumlazimu kununua vingi ili vitosheleze.

Naye Mkazi wa Salasala, Mwajabu Abdul, mwenye watoto watatu anayefanya kazi ya saluni, alisema hali hiyo inawalazimu kutokula chakula cha mchana ili kuepuka gharama kubwa kutokana na kuwa na kipato kidogo.

"Wakati mwingine unajikuta umeamka na Sh. 5,000, hivyo kuigawanya upate miko mitatu si rahisi. Tunachofanya na wanangu tunachemsha mihogo ya buku (Sh. 1,000) tunakunywa na chai saa tano asubuhi. Tukishashiba tena tunakuja kupika chakula saa 11:00 jioni, tunakula saa moja tunalala, siku zinasogea," alisema.

Mwajabu alisema awali walipata shida kwa sababu walikuwa wameshazoea kula milo mitatu hali iliyosababisha watoto kulegea na kusinzia wakati wa mchana lakini sasa wameshazoea na maisha yanakwenda sawa.

Dereva wa bodaboda eneo la Mwenge, Alex Mushi, alisema alichukua uamuzi wa kutokula chakula cha mchana baada ya kugundua kuwa anatumia pesa nyingi kula kwa mama ntilie.

"Kwa siku nikipata sana katika biashara yangu ni Sh. 25,000. Hapo Sh. 10,000 ni ya mwenye bodaboda, nabaki na Sh.15,000. Asubuhi chai tu Sh. 2,500, mchana ili ushibe lazima ule pande mbili za ugali maana unapimwa kidogo sana jumla Sh. 4,000. Jioni pia utumie Sh. 4,000 jumla Sh. 10,500 bado hujanywa maji. Sioni hata dalili ya kununua kiwanja," alisema.

Kutokana na kupanda huko kwa bidhaa, Mushi alisema kuna haja ya serikali kuangalia namna ya kupunguza gharama za nafaka kwa kuwa ndizo inasababisha gharama za vyakula kupanda huku watu wa hali ya chini wakiathirika zaidi.

Nipashe ilifunga safari mpaka kwa wauzaji wa vyakula ambapo Angela Maganga, muuzaji wa vitumbua Temeke, alisema amepoteza baadhi ya wateja baada ya kupunguza kipimo cha vitumbua ili apate faida kutokana na kupanda gharama za nafaka na mafuta ya kupikia.

Alisema ndani ya mwaka mmoja kilo moja ya mchele wa vitumbua imepanda kutoka Sh.1,400 hadi Sh.2,000 na mafuta lita moja ilikuwa Sh. 3,500 sasa Sh.5,000.

"Ni kweli dada nimepunguza kipimo cha upawa ili na mimi nipate faida nihudumie familia yangu, ndicho kimewakimbiza wateja. Serikali iangalie hizi nafaka mbona zinazopanda kila kukicha na zinaelekea kuua biashara zetu ambazo ndizo tunategemea kusomesha watoto," alisema.

Naye Maria Kallaghe, mamalishe katika soko la Tandale, alisema kitendo cha wateja katika eneo hilo kutokula chakula cha mchana, kimemrudisha nyuma kimaendeleo kwa sababu anapata faida nusu ya aliyokuwa anapata mwanzo.

"Mauzo yameshuka kutoka Sh. 50,000 hadi Sh. 30,000. Hapo nikitoa hela ya mtaji najikuta napata Sh. 10,000 faida na inategemea na siku. Ukiamka ukakuta mchele umepanda hapo tena faida inazidi kupungua. Kwa ufupi maisha ni magumu," alisema.

**SERIKALI IKO KAZINI**

Agosti 15, mwaka huu, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alipozungumza jijini Dodoma, alisema serikali inaendelea kuchukua hatua ili kuwapunguzia wananchi athari zitokanazo na kupanda kwa bei ya bidhaa muhimu.

Alisema hatua hizo ni pamoja na kuwapunguzia gharama za uzalishaji, uagizaji na usambazaji wa bidhaa, ili kuleta uhimilivu wa bei kwenye soko lengo likiwa kumlinda mlaji kwa kuhakikisha anapata bidhaa bora kwa bei stahiki na kuzuia upandishwaji holela wa bei za bidhaa.

Pia alisema serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa wazalishaji wa mbolea kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji, hivyo kuleta unafuu wa bei ya mazao muhimu ya chakula pamoja na kupunguza ushuru kwa maroli yanayosafirisha bidhaa.

Ripoti ya Shirika la Ushirikiano na Maendeleo ya Uchumi (OECD), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), kuhusu Mtazamo wa Kilimo 2022-2031 inaonyesha mazao ya kilimo kote duniani yatakabiliwa na changamoto za kimsingi kwa miaka 10 ijayo na kuzitaka nchi kuchukua hatua endelevu kukabiliana na changamoto hiyo.

Ripoti hiyo inaeleza changamoto hizo ni kupanda kwa bei za mazao ya kilimo kulikosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona, hali mbaya ya hewa katoka nchi muhimu za utoaji wa mazao, kupanda kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji na uuzaji usio na uhakika wa mazao ya kilimo kutoka Ukraine na Russia ambazo ni nchi muhimu zaidi za utoaji wa nafaka umeifanya hali ya hivi sasa izidi kuwa mbaya.

# Samia apanda boti Zanzibar hadi Dar, alipa nauli kamili

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alisafiri kwa boti kutoka Zanzibar hadi Dar es Salaam kwa kulipa nauli, hivyo kuwa mkuu wa nchi wa kwanza kutumia usafiri huo.

Licha ya kutumia usafiri huo, Rais Samia alipita katika njia wanazotumia abiria wengine.

Jana mchana, zilisambaa picha mtandaoni zikimwonyesha Rais akiwa ndani ya boti hiyo huku akiwasalimia abiria wa daraja la kwanza, la pili na la tatu jambo ambalo liliwafurahisha wasafiri hao.

Pia mtandaoni kulikuwa na mjadala huku wengi wakipongeza na kueleza kuwa ameweka historia ya kuwa kiongozi wa kwanza kutumia usafiri huo kwa kuwa wengi wanatumia ndege kwenda na kurudi visiwani humo.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Kampuni ya Azam Marine, Ally Mohammed Abeid, alisema Agosti 29, mwaka huu, walikuja watu wakaomba kukata tiketi kwa ajili ya kiongozi fulani kusafiri na waliweka 'booking' na ilipofika Septemba 3, walilipia nafasi zote walizokuwa wameshikilia lakini hawakueleza ni kiongozi gani.

"Walikata madaraja ya VIP Royal na Economy. Rais akiwa na watu wake walipita kwenye utaratibu wa kawaida hadi kuingia kwenye boti ingawa abiria anaweza kwenda moja kwa moja hadi kwenye daraja lake lakini alitoomba atembelee madaraja yote kusalimia wananchi.

"Tumefurahi sana kuwa boti ya kwanza kumsafirisha Rais, tumepata CV (wasifu) nzuri sana kwa mara ya kwanza kumsafirisha Rais tena kawaida kabisa. Hakukuwa na usumbufu wowote zaidi ya ulinzi mkali. tumejisikia faraja sana," alisema Abeid.

Aidha, aliwataka viongozi wengine wa serikali wanaopenda kusafiri kwa ndege pia kutumia usafiri unaotumiwa na wananchi ambao utawafanya wajifunze mambo mengi zaidi.

Chollo Master aliandika: "Mama ana upendo mwingi sana kwa wananchi hakika ni kipenzi cha watu." Naye Mtamaushi aliandika: "Mama hana tatizo, tatizo lipo kwa walafi wanaomzunguka."

Mwingine anayejiita Nchi Yangu Nzuri, aliandika: "Tunataka kuona Rais na timu yake nzima wakibana matumizi kila kona kwani hata nyumbani kwako hali ikiwa mbaya hauwaonyi ndugu maskini kwa mabavu au kukopa kupitiliza. Unabana matumizi yako ya maisha ya raha) na kuweka vipaumbele vya muhimu kama watoto kusoma, afya na maendeleo."

Mwingine anayejiita Tanzanian Bitter Leaf aliandika: "Safi, tunapenda kuona viongozi wako inclusive (jumuishi) na wanaoishi kwa mifano kwa kuwa karibu na wananchi ili kujua matatizo yao na kuyashughulikia."

Katika moja ya makundi songezi, mwandishi mkongwe na blogger, Maggid Mjengwa, aliandika: "Haijapata kutokea kwenye Jamhuri yetu. Katika kuishi kwangu, kusoma na kufuatilia mambo, ni mara ya kwanza leo (jana) kusoma na kuona picha ikimwonyesha Rais akipanda boti kutoka kisiwani kwenda bara."

Alisema kumwelewa kiongozi zaidi ni pale anaposhuka jukwaani na kwamba yako ya kutafsiri hasa inapohusu shida na changamoto wanazopitia watu wake si tu anazijua bali amezipitia.

"Naamini anachofanya wala si maigizo bali ni kushuka chini kujionea, kusikiliza, kujifunza na kujenga uelewa mpana utakaosaidia kwenye kutoa mwelekeo sahihi wa njia anayowapitisha watu wake. Kuyafanya hayo bila mbwembwe, majigambo na yote yenye kuendana na mamlaka makubwa aliyo nayo.

"Nakumbuka mwaka mmoja akiwa Makamu wa Rais, alishiriki matembezi ya miguu kuhamasisha kampeni ya kupambana na maradhi yasiyo ya kuambukiza. Nilishiriki matembezi yale yaliyoishia viwanja vya Leaders.

"Mwisho wa matembezi yale na mbele ya Mzee Mwinyi, Samia akizungumzia changamoto za huduma za afya na husan kwa kinamama, alisimulia kisa cha yeye kabla ya uheshimiwa.

"Kuna siku akiwa kwenye daladala na mtoto mgonjwa mgongoni, na akiwa amesimama njia nzima, daladala lile lilimshusha eneo la Kariakoo, Hapo Samia na mwanawe mgongoni anasimulia alivyotembea kwa miguu kutoka Kamata mpaka Hospitali ya Mnazi Mmoja," alisema.


Kwa mujibu wa Mjengwa, alichofanya Rais kinahusu kuzielewa, kuziishi na kuzitafutia majawabu mujarab shida za anaowaongoza.

"Kwa nini basi baadhi ya viongozi husahau haraka walikotoka, kudhihaki wanaowaongoza na kutoonea uchungu matumizi yalo ukwasi?" Alihoji.

## HABARI KITAIFA

# Raila Odinga akubali matokeo

**Na Waandishi Wetu**



SAA chache baada ya Mahakama ya Juu nchini Kenya kuhalalisha ushindi wa Rais mteule William Ruto kwenye uchaguzi uliofanyika mwezi uliopita, mpinzani wake kutoka Chama cha Muungano wa Azimio la Umoja, Raila Odinga,(Pichani) amekubali matokeo hayo.

Hata hivyo, alisema hakuridhishwa na hukumu hiyo kwa madai kuwa mawakili wake walitoa hoja zenye mashiko na kujitosheleza.

Taarifa iliyotolewa na sekretariati ya urais ya mgombea huyo ilieleza kushangazwa na hoja tisa zilizotolewa na mawakili wake kukataliwa na mahakama.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa hukumu hiyo sio mwisho wa harakati zao za kuibadilisha nchi hiyo kuwa yenye kuzingatia misingi ya kidemokrasia.

Hukumu hiyo iliyosomwa na Jaji Mkuu, Martha Koome, ilitupilia mbali madai tisa ya kupinga matokeo ya urais kutoka kwa mgombea wa Muungano wa Azimio la Umoja Odinga dhidi ya ushindi wa Ruto.

Kwa mujibu wa jaji huyo katika hukumu aliyoisoma kwa niaba ya jopo la wenzake saba, na kuchukua zaidi ya saa moja na nusu alikubaliana na ushindi wa Ruto akisema madai dhidi yake kutoka kwa Raila yalikuwa batili kwa kukosa ushahidi unaojitosheleza.

Jaji Mkuu Koome, alihalalisha ushindi wa Ruto alioutaja umefanikiwa kukidhi hitaji la ushindi kisheria unaovuka asilimia 51, pia Tume ya Uchaguzi Kenya ilitumia taratibu sahihi za kisheria aliyoifafanua 'kupata asilimia 64.4 ya wapigakura'.

Pia, alisema Mahakama haikupata ushahidi uliotolewa kuonesha kuwa Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati na wafanyakazi wengine wa IEBC walihusika kuchakachua matokeo na kwamba mamlaka ya kuthibitisha na kujumlisha matokeo ya uchaguzi wa urais hayatokani na mwenyekiti bali tume.

Kuhusu makamishna wanne walioinga matokeo ya mwisho, alisema walishiriki uhakiki wa awali na kujumlisha matokeo na hawakutoa hati yoyote inayoonesha matokeo yalibadilishwa wala kueleza ni kwanini walishiriki katika mchakato wa uhakiki ambao walisema haukuwa wazi.

Kuhusu kuingiliwa kwa tovuti ya matokeo, alisema hakukuwa na ushahidi wa mtu kuingilia mfumo wa utumaji matokeo kwa lengo la kuvuruga matokeo na kuwa Tume ilieleza jinsi mfumo ulivyonasa fomu za matokeo zilizowekwa katika tovuti yake na zote zilikuwa sawa na zilizowasilishwa katika kituo kikuu cha kuhesabia kura.

Vilevile, hakukuwa na ushahidi wa fomu za uchaguzi katika tovuti ya matokeo ya mtandaoni zilibadilishwa kutoka kwa zile za awali zilizochapishwa na kuwaonya mawakili wanaowasilisha ushahidi wa kupotosha au kubuniwa husababisha kesi kuwa ndefu.

**RUTO: KENYATTA SWAHIBA WANGU**

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema mtangulizi wake Uhuru Kenyatta ni swahiba wake na amemkaribisha kwa mipango ya pamoja.

Alisema katika urafiki wao, daima hawajawahi kuwa na maagano ya kushirikiana kisiasa mbele ya safari.

Pia alikimwagia sifa kikosi cha wanasheria waliompatia ushindi katika hukumu iliyotolewa jana, huku akisifu uweledi wa mahakama.

Ruto aliyekuwa na tabasamu kila wakati alimkaribisha mpinzani wake Raila, wajipange pamoja kujadili namna ya kutekeleza miradi endelevu ambayo ilikuwa haijakamilika.

Pia aliahidi daima kumpa heshima Odinga katika Kenya anayoitaja inazingatia utawala wa sheria.

Mmoja wa wafuasi wa Ruto kutoka mji wa Bondo, katika jimbo la CI-a, Jaroo Pajama, alisema kuwa anamshukuru Mungu kwa kuwa haki imetendeka na anaamini rais huyo atakwenda kutatua changamoto ya kupaa kwa bei ya chakula katika nchi hiyo.

Wakati Solomon Tirop, kutoka Sugoi alisema ana furaha kuona timu ya majaji sita imetoa uamuzi ulio sahihi na kuidhinisha mamlaka iliyo sahihi kuchukua dola na kuwa uchaguzi ulikuwa wa uhuru, amani na wenye haki.

**WANASIASA WANENA**

Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alisema kilichofanyika nchini Kenya sio tu katiba bali ni ukatiba, huku akielekeza kuwa wamejifunza uwazi na kwamba Kenya ni kati ya nchi chache duniani zenye uwazi mkubwa.

Alisema Kenya ni moja ya nchi pia ambazo zitakuwa na uchumi mkubwa kutokana na uwazi uliopo, akitoa wito kwa nchi nyingine barani Afrika na duniani kwa ujumla kuiga mfano huo.

"Kenya hakuna mshindi, tofauti ya matokeo ni ndogo sana ila kilichoshinda ni amani ya iliyopo Kenya, wito wangu waendelee kuwa pamoja, Tanzania ili tuvuke tuige mfano wa wenzetu," alisema Mbatia.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, alisema uamuzi uliotolewa na mahakama ya juu nchini Kenya ya kuazimia uteuzi wa Ruto na kutupilia mbali mashtaka ya Odinga ulifanyika kwa uwazi na haki.

"Mahakama ya Kenya imetoa funzo kwa Tanzania katika kuharakisha mchakato wa Katiba Mpya," alisema Mnyika.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema kilichotokea nchini Kenya kuhusu maamuzi ya mahakama ya juu ni suala la kuigwa, huku akidai kuwa ni wakati kwa Tanzania kusisitiza kuwa na tume huru na uwazi katika uendeshaji wa uchaguzi.

Ruto alitangazwa na Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati, kuwa Rais mteule baada ya kupata kura 7,176,141 (asilimia 50.49) dhidi ya 6,942,930 za Odinga (asilimia 48.85) ), huku Prof. George Wajackoyah wa Roots Party akipata kura 61,969 (asilimia 0.44) na David Mwaure Waihiga wa Agano Party akiibuka wa nne kwa kura 31,987 (asilimia 0.23).

# Adaiwa kumuua babake kwa kushindwa kumtafutia mke

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

POLISI inamshikilia Kristatus Victory (23), mkazi wa Lukuledi wilayani Masasi kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi Victory Milanzi (74), kwa kumchoma kisu mdomoni na tumboni na kumjeruhi mama yake mzazi Carolina Ludugeli (68) kwa madai ya kushindwa kumtafutia mchumba wa kuoa.

Akithibitisha, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, ACP Issack Mushi, alisema tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki na mtuhumiwa anashikiliwa kwa mahojiano.

Alisema upelelezi utakapokamilika mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani ili kujibu tuhuma zinazomkabili.

Mtendaji wa kijiji hicho, Kevin Milanzi akizungumza na gazeti hili alisema tukio hilo lilitokea saa mbili usiku katika Kijiji cha Lukuledi baada ya kijana huyo kwenda kwa wazazi wake na kuwashambulia kwa kisu na panga.

Alisema baba wa kijana huyo alikuwa nyumbani kwake na mkewe amejipumzisha kabla ya mtoto wao kufika na kuanza kumshambulia kwa kumchoma kisu.

Taarifa za awali kutoka ndani ya familia zinadai kuwa kijana huyo aliwaagiza wazazi wake wamtafutie mchumba wa kufunga naye ndoa na alipoona agizo lake halitekelezwi ndipo alipochukua uamuzi huo.

Mtendaji huyo alisimulia kuwa kijana huyo ana utamaduni kila ikifika usiku kwenda kwa wazazi wake kupata chakula na kurudi nyumbani kwake anakoishi Mtaa wa Kilimani.

Alisema tukio hilo limemshangaza kila mtu na wakati kijana huyo akimshambulia baba yake, mke wa Victory (mama wa mtuhumiwa) alijaribu kumwokoa mume wake ndipo naye alipojeruhiwa kwa kupigwa na panga mikononi.

Milanzi alidai, baba alipozidiwa alianguka chini ndipo kijana huyo alipomgeukia mama yake na kuanza kumpiga na upanga na kumjeruhi mikononi.

"Wananchi wa Lukuledi walimsaka kijana huyo usiku huo huo na kufanikisha kumkamata na kumpeleka katika kituo cha polisi," alisema Milanzi.

Mama wa mtuhumiwa akisimulia tukio hilo, alisema alisikia sauti ya mume wake akipiga mayowe sio ya kawaida na alipoingia ndani ya chumba alimkuta mtoto wake akiwa amemweka kisu mdomoni baba yake ambaye wakati huo alikuwa akivuja damu.

Alisema alipojaribu kumsogolea, mtoto wake alimpiga kwa kutumia kisu na panga na kulazimika kuomba msaada kwa majirani kumsaidia mume wake ambaye alikuwa ameshapoteza maisha.


**IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATED) OF NYAMAGANA DISTRICT AT MWANZA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 17 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GERALD OTIENO NJURA DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR THE GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION BY JUDITH KENZANILA NJURA**
**INVENTORY OF ESTATE**
**(Section 107, Rule 106)**
**Date of Grant: 15th Day of October 2021**

| ASSETS | LIABILITIES |
|---|---|
| Item No. Description of Property Value | Item No Description Value |
| •Immovable Propertie NIL | Names of creditors NIL |
| •NSSF Contribution 68,000,000/= | Mortgages NIL |
| •Shares at Elimu Welfare SAUT NIL | Other depts. NIL |
| •Share at UMOJA WA KUSAIDIANA NIL | Death bed expenses NIL |
| •Gratuity at SAUT NIL | Funeral expenses NIL |
| •Stock and shares NIL | Total.........TZS 68,000,000/= |
| •Insurances police NIL | |
| •Interest in business NIL | |
| •Book depts. NIL | |
| •Furniture NIL | |
| •Personal effects NIL | |
| •Other properties NIL | |

**I JUDITH KENZANILA SARAPION** the administratrix of the estate of the late **GERALD OTIENO NJURA** hereby certifies that the foregoing inventory of the said estate is true to the best of my knowledge, information and belief.

Dated at Mwanza this............Day of August 2022.........

**SIGNATURE OF THE ADMINISTRATRIX**

Field in court this..................Day of..........................2022

..........................................
**DISTRICT DELEGATE**
**Drawn and field By:**
**Peter H.Kipfumu (Advocate)**
**P.O.BOX 44**
**Handeni- Tanga**
**Tanzania**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
05 - 09 - 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatano tarehe 07 - 09 - 2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zenye namba za usajili:
**T 203 DYJ / T 887 DJB T 135 CCP / T 837 DJB T 908 DSD / T 156 CHN T 985 DTN / T 153 CHN T 245 BXH / T 837 CHK**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 22** |
| **Upana** | - | **mita 4.5** |
| **Kimo** | - | **mita 5.0** |

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217030702

# Mwinyi akerwa wizi mabilioni serikalini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameonesha kukerwa na wizi wa mabilioni ya fedha katika serikali na kuahidi kuteua Mkurugenzi Mkuu mpya wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), baada ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Ahmed Makarani kujiuzulu.

Alisema baada ya uteuzi huo atampa kazi maalum ikiwamo kumkabidhi Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ili hatua madhubuti zichukuliwe fedha hizo zirudi na wahusika wachukuliwe hatua.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Ikulu, alisema mkurugenzi atakayemteua atachukua hatua madhubuti kwa waliohusika wote kwenye wizi wa fedha na ubadhirifu wa mali za serikali waliotajwa katika ripoti ya CAG.

Dk. Mwinyi alimpongeza Mkurugenzi wa ZAECA, kwa kujiuzulu kutokana na udhaifu katika mamlaka hiyo na kuwajibika kwake.

Akizungumzia ripoti ya CAG iliyowasilishwa kwake, alisema yaliyowasilishwa katika ripoti hiyo ni ya ukweli na kuna mambo ambayo yanasababisha kutokea kwa ubadhirifu wa mali za umma. Alitaja miongoni mwa sababu kuwa ni usiri wa kuficha taarifa za CAG, sababu iliyomfanya kuandaa utaratibu wa kuwapo kwa uwazi na ukweli wa uwasilishwaji wa taarifa hiyo ili kila mmoja apate taarifa.

Ubadhirifu mwingine ni baadhi ya watendaji wa serikali kusababisha fedha kupotea au mifumo ya ukusanyaji mapato kutokuwa sawa na kutokuwapo kwa uwajibikaji.

Rais Mwinyi, alisema atahakikisha anatafuta ufumbuzi wa kasoro zilizojitokeza katika taarifa ya CAG ikiwamo kuwachukulia hatua wote waliohusika na wizi wa fedha za serikali, kujenga weledi kwa watendaji na mifumo ya taasisi.

"Lazima tuziunde upya taasisi zetu ikiwamo ZAECA na lazima kuijenga kuwa endelevu ili kufanya kazi zake kwa ufanisi kwa sababu fedha nyingi zimeibiwa na wapo walioiba wamekiri, lakini hawajachukuliwa hatua," alisema.

Aliagiza fedha zote zilizoibiwa au kupotea serikalini, wahusika wawajibishwe na kuitaka Taasisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuwa madhubuti kupeleka kesi mahakamini ili haki itendeke.

Alifafanua kuwa lazima kila hoja iliyotolewa na CAG ifuatiliwe kwa kina na waliohusika na ubadhirifu wa mali za umma waibuliwe na wachukuliwe hatua stahiki.

Akizungumzia ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo katika wilaya zote za Unguja na Pemba, alisema amefarijika na ujenzi wa miradi inayoendelea kujengwa.

"Nimefarijika na miradi ya maendeleo inayoendelea kujengwa ambayo nimeikagua katika ziara yangu na imekua na mafanikio," alisema.

Kuhusu marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma alisema ameongeza kiwango cha mishahara ili utendaji wa kazi uimarike.

Aliwataka watendaji wa umma kutekeleza wajibu wao na anatarajia kuanza ziara za kushtukiza katika taasisi za serikali ili kurejesha nidhamu na kila mmoja kuwajibika.

Akitoa taarifa za vijana wa Zanzibar wanaopotea katika mazingira ya kutatatisha kwa madai ya kuhusishwa na vikundi vya waasi, alisema serikali itafanya utafiti ili kubaini tuhuma hizo.



Mkurugenzi wa Radio One/Capital Radio, Deogratius Rweyunga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa gari mpya itakayotolewa kwa mshindi atakayeshiriki bahati nasibu ya mchezo Supa inayoendeshwa na Radio One. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA ITV, Moses Fumbuka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Radio One kutoa zawadi ya gari mshindi wa SUPA

**Na Waandishi Wetu**

KITUO cha Radio One kwa kushirikiana na Capital Radio kimetangaza zawadi ya gari aina ya Toyota IST kwa mshindi atakayeibuka katika mchezo wa SUPA unaoendeshwa na vituo hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Radio One, Deogratius Rweyunga, alisema mshindi atakabidhiwa gari hiyo yenye thamani ya Sh. milioni 15.

Rweyunga alisema hiyo ni mara ya kwanza kwa zawadi hiyo kutolewa tangu kuanzishwa kwa mchezo huo miezi kadhaa iliyopita.

Alisema lengo la mchezo huo ni kutatua tatizo la ukosefu wa mitaji kwa vijana, akibainisha kuwa mtu atakayeshinda anakwenda kubadilisha maisha yake.

"Tumeamua kuanzisha mchezo huo ili kuwawezesha vijana kujikwamua na tatizo la mitaji, ndani ya miezi minne watu mbalimbali wameshuhudia kupitia Radio One na Capital Radio, mchezo huo ulivyobadili maisha yao wakiwamo mama ntilie, wakulima na vijana."

Alibainisha tangu mchezo huo ulipoanza hadi sasa watu kadhaa wamenufaika kwa kujipatia viwango mbalimbali vya fedha kuanzia Sh. 100,000 hadi Sh. 1,000,000, pikipiki yenye thamani ya Sh. milioni 2.6 na Smart TV.

Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa Kituo cha Televisheni cha ITV, Moses Fumbuka, alifafanua jinsi ya kucheza mchezo huo kupitia mitandao mbalimbali ya simu kwa wanaotaka kushinda gari kwa kusikiliza vipindi vya Radio One wakiwa na laini za simu za mitandao ya Tigo, Vodacom, Airtel na Halotel.

Alisema kwa Sh. 1,000 pekee atabonyeza namba za menyu kulingana na mtandao wanaotumia, kisha kwenda lipa bili, halafu kuingiza namba ya kampuni ambayo ni (222223) na baada ya hapo wataingiza kumbukumbu namba ambazo ni (111), au neno SUPA.

"Kwa gharama ya Sh. 1,000 unaweza kujishindia fedha taslimu kila siku na pikipiki yenye thamani ya shilingi milioni 2.6 kila mwisho wa wiki (ijumaa) kupitia Capital Radio na mwisho wa mwezi wa tisa unaweza kujishindia gari mpya aina ya Toyota IST yenye thamani ya Sh. milioni 15 kupitia Radio One."

Mtangazaji wa Radio One anayefanya kipindi cha DJ Show, Dolores Kobe, alisema mchezo huo ni wa kielektroniki, mtu yeyote anaweza kushinda.

Aliwasihi Watanzania kucheza mchezo huo muda wote ili waweze kushinda zawadi hizo.

## Ofisa mikopo kortini madai ya kuingilia mifumo ya kompyuta

**Na Pilly Kigome**

OFISA Mikopo wa Kampuni ya Platinum Credit Tanzania, Mulokozi Muyeko (34) na wenzake watano, wamependishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Kisutu kwa madai ya kuingia kwenye mifumo ya kompyuta ya kampuni hiyo isivyo halali.

Mbali na Muyeko wengine ni raia wa Kenya, Samwel Mwasya, Rajabu Msangi, Rajabu Muawia, James Kay na Frank Saka.

Wakili wa Serikali, Tumain Mafuru, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Yusto Ruboroga, kuwa kati ya Aprili Mosi, 2022 na Julai 20, 2022 eneo lisilojulikana ndani na nje ya Tanzania, washtakiwa wote kwa pamoja walifanya kosa la kuingilia mifumo isiyo kihalali.

Mafuru alidai kuwa katika shtaka la pili, tarehe hiyo hiyo, washtakiwa wote wakiwa maeneo yasiyojulikana ndani na nje ya Tanzania, kwa makusudi na kusikokuwa na uhalali, waliingia kwenye mifumo ya kampuni hiyo.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa tarehe hiyo katika kampuni hiyo, iliyoko Barabara ya Ally Hassan Mwinyi, Muyeko alisambaza nywila kwa Salum Msuya na Frank Saka na kumsababishia kuingia kwenye mifumo ya kompyuta na kuweza kufanya udukuzi.

Mafuru alidai shtaka la nne tarehe hiyo hiyo maeneo hayo mshtakiwa Muawia na Saka waliingia kwenye mifumo pasipo kuwa na uhalali.

Katika shtaka la tano, washtakiwa wote kwa pamoja kwa makusudi bila kuwa na uhalali wowote waliingilia katika mifumo ya kampuni hiyo.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka yao, Hakimu Ruboroga alisema kila mshtakiwa anatakiwa awe na wadhamini wawili watakaosaini bondi ya Sh. milioni tano na pia wawe na vitambulisho vinavyotambulika ikiwamo cha taifa.

Muyeko, Mwasya na Saka wameshindwa kutimiza masharti ya dhamana wamerudishwa rumande na mshtakiwa Msangi, Muawia wametimiza masharti hayo na wako nje kwa dhamana.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Septemba 15, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

## Kigogo reli akutwa na kesi ya kujibu

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Hodhi ya Mali za Shirika la Reli (RAHCO), Benhardard Tito, amepatikana na kesi ya kujibu katika kesi ya matumizi mabaya ya madaraka inayomkabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Aidha, Mahakama hiyo imewaachia Mwanasheria wa RAHCO, Emmanuel Massawe na mfanyabiashara ambaye ni mwakilishi wa kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Limited, Kanji Mwinyijuma, baada ya kutokuwakuta na kesi ya kujibu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga, baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi tisa wa upande wa Jamhuri na vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani dhidi ya washtakiwa hao.

Ngimilanga alisema ushahidi uliotolewa haukumgusa mshtakiwa wa pili (Massawe) na Mwinyijuma, kwa hiyo mahakama haijawakuta na kesi ya kujibu, hivyo Tito pekee ndiye anatakiwa kujitetea kwa sababu amepatikana na kesi ya kujibu.

Kutokana na kukutwa na kesi ya kujibu, Tito anatarajia kuanza kujitetea Oktoba 13, mwaka huu.

Awali, Wakili wa Serikali, Iman Nitume, aliieleza mahakama kuwa kesi imeletwa kwa ajili ya uamuzi na wako tayari kwa uamuzi huo.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka manane yakiwamo uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, kula njama na kuisababishia RAHCO hasara ya Dola za Marekani 527,540.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Septemba Mosi, 2014 na Septemba 30, 2015 kwa nia ya kutenda kosa, walikula njama kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Ilidaiwa kuwa Februari 27, 2015 katika ofisi za RAHCO zilizoko, Ilala jijini Dar es Salaam, Tito alitumia madaraka yake vibaya kwa kuijairi Kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Ltd kama mshauri wa mradi wa uimarishaji reli ya kati bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya RAHCO.

Ilidaiwa kuwa Tito na Massawe, Machi 12, 2015 katika ofisi za RAHCO, wakiwa katika nyadhifa zao, walitia saini barua ya kuihalalisha kampuni hiyo ya Afrika Kusini kuwa mshauri wa mradi wa uimarishaji reli ya kati na kutoa huduma za ushauri wa kifedha kuhusu mradi huo.

Katika shtaka lingine, ilidaiwa kuwa Tito na Massawe, Machi 12 na Mei 20, 2015 wilayani Ilala walishindwa kuwasilisha mkataba wa huduma ya ushauri kati ya kampuni hiyo ya Afrika Kusini na RAHCO.

Tito na Massawe wanadaiwa Mei 20, 2015 katika ofisi za RAHCO, kwa kutumia madaraka yao vibaya, walitia saini mkataba wa kutoa huduma za ushauri na kampuni ya Afrika Kusini bila ridhaa ya Bodi ya Zabuni ya RAHCO.

# Mwili wa Askofu aliyefariki baada ya kuanguka madhabahuni waagwa

**Na Steven William,** MUHEZA

MAMIA ya wananchi jana walijitokeza kuuaga mwili wa aliyekuwa Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa, George Chiteto, aliyefariki dunia Jumamosi iliyopita.

Askofu Chiteto alikutwa na mauti muda mfupi baada ya kumaliza mahubiri katika Kanisa la Kristo Mfalme Mtaa wa Madaba, Muheza mkoani Tanga, baada ya kumaliza mahubiri na kuzidiwa kabla ya kupelekwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza.

Chiteto alikuwa akihubiri kwenye ibada ya mazishi ya Rais wa Ushirika wa Mama wa Kikristo Kanisa la Anglikana Tanzania( UMAKI), Hilda Lugendo, ambaye alizikwa kijiji cha Mbwego kata ya Mkuzi. Hilda alikuwa mke wa Julius Lugendo, Askofu wa Anglikana Dayosisi ya Southern Highlands, Mbeya.

Ibada ya mazishi ya kiongozi huyo ilihudhuriwa na waumini, viongozi wa kanisa na serikali iliongozwa na Askofu Mkuu wa Anglikana Tanzania, Dk. Maimbo Mndolwa, nyumbani kwa ndugu wa marehemu, Elisha Cheti, eneo la Genge na kanisa la Kristo Mfalme Mtaa wa Madaba.

Baada ya ibada hiyo, safari ya kwenda Mpwapwa mkoani Dodoma ilianza ikiongozwa na Askofu Mstaafu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Tanga, Dk. Philip Baji.

Akihubiri kwenye ibada hiyo, Askofu Mkuu Mndolwa alisema kanisa limepoteza mtu muhimu lakini Mungu amempenda, hivyo hakuna cha kufanya.

Aliwakumbusha wakristo kuendelea kumcha Mungu, ili wajiwekee njia ya kupata pepo huko mbinguni kwa kuwa siku moja wataonja mauti.

Katika ibada hiyo maaskofu kutoka madhehebu mbalimbali Tanzania walihudhuria kuuwaga mwili huo na kutoa ujumbe mbalimbali wa neno la Mungu katika msiba huo mkubwa wa kitaifa.

Chiteto (59) alifariki dunia akiwa amekaa katika nafasi hiyo kwa siku sita tu baaada ya kuwekwa wakfu Agosti 28, mwaka huu kuwa Askofu wa Tatu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa. Waliomtangulia ni Askofu Dk. Simon Chiwanga na Askofu Dk. Jacob Chimeledya.

Askofu Chiteto ameacha mke na watoto sita. Kabla ya kuchaguliwa kuwa askofu Juni 26, mwaka huu, alikuwa Mhadhiri wa Theolojia katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana (SJUIT), Dodoma kinachomilikiwa na Kanisa la Anglikana Tanzania.



Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Mahimbo Mndolwa (kushoto), akiwaelekeza wachungaji jana sehemu ya kuweka jeneza lenye mwili wa aliyekuwa askofu wa Dayosisi ya Mpwapwa mkoani Dodoma, George Chiteto, aliyefariki dunia wilayani Muheza mkoani Tanga kwa ajili ya ibada ya maziko. PICHA: STEVEN WILLIAM

# Majaliwa ataka uadilifu ujenzi mji serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa Mji wa Serikali kuzingatia uadilifu katika matumizi ya fedha ili ukamilike kwa wakati na kwa viwango.

Pia amewaagiza makatibu wakuu wa wizara zote ambazo baadhi ya watumishi bado wako Dar Es Salaam, wahakikishe wanahamia Dodoma kama ilivyoelekezwa na serikali.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana baada ya kukamilisha ziara yake ya kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Mji wa Serikali, Mtumba jijini Dodoma. Aliwashukuru na kuwapongeza makandarasi wanaojenga mji huo.

"Dhamira ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha ujenzi wa Makao Makuu unaendelea vizuri ni nzuri na lazima tujivunie maono ya viongozi na kazi nzuri wanayoifanya pamoja na kazi nzuri za wataalamu wetu," alisema.

Majaliwa alisema ujenzi wa mji wa serikali utakuwa wa kisasa kwa kuwa utaendeshwa kidijitali. "Fedha za kutekeleza haya zipo na ninawahakikishia kila kitu kitakamilika. Dhamira ya Rais Samia ni kufanya makao makuu kuwa bora zaidi," alisisitiza.

Kadhalika, Majaliwa aliwasisitiza vijana wa Kitanzania wanaofanya kazi katika mradi huo, waendelee kufanya kazi kwa kuzingatia weledi, uadilifu na waendelee kuzingatia maelekezo wanayopewa viongozi wao ili wawe na uwezo wa kujenga na kusimamia kazi zao.

Majengo ambayo yamekaguliwa ni Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu linalojengwa na SUMA JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 22.8. Ujenzi wake ulianza Oktoba 11, mwaka jana na unatarajiwa kukamilia Aprili 17, mwakani. Jengo hilo lenye sakafu sita, ujenzi wake umefikia asilimia 46.

Jengo lingine ni Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu lenye sakafu sita linalojengwa na SUMA JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 18.62. Ujenzi wake umefikia asilimia 47, ulianza Oktoba 18, mwaka jana na unatarajiwa kukamilia Aprili 17, mwakani.

Pia alikagua ujenzi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) lenye sakafu sita pia linalojengwa na kampuni ya M/S Corporation kwa gharama ya Sh. bilioni 20.29. Ujenzi wake umefikia asilimia 54, ulianza Oktoba 15, 2021 na unatarajiwa kukamilia Oktoba 14, mwakani.

Jengo lingine lililokaguliwa ni Wizara ya Maliasili na Utalii linalojengwa na kampuni ya M/S Li Jun Development Construction Company Limited kwa gharama ya Sh. bilioni 16.41. Ujenzi wake umefikia asilimia 69 ambao ulianza Novemba 23, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Novemba 22, mwakani.

Pia Waziri Mkuu alikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Mwanasheria Mkuu wa Serikali linalojengwa na SUMA JKT kwa gharama ya Sh. bilioni 26.81. Ujenzi wa jengo hilo la sakafu tano umefikia asilimia 42 na ulianza Septemba 9, mwaka jana, unatarajiwa kukamilika Septemba 15, mwaka ujao.

Mradi mwingine uliokaguliwa ni wa jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi linalojengwa na Shirika la Nyumba la Taifa kwa gharama ya Sh. bilioni 22.30 na umefikia asilimia 45.05, ujenzi huo ulianza Oktoba 15, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Oktoba 14, mwakani.

Pia alikagua ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora linalojengwa na Wakala wa Majengo Tanzania kwa gharama ya shilingi bilioni 21.64. Ujenzi huo wa jengo la sakafu sita, umefikia asilimia 54. Ulianza Septemba 21, 2021 na unatarajiwa kukamilika Machi 20, mwakani.

Awali, Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Mji wa Serikali, Meshack Bandawe, alisema awamu ya pili ya ujenzi wa mji huo ilianza Oktoba, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwakani. Alisema mradi huo unahusisha majengo 25 ya wizara pamoja na mawili ya taasisi za umma.

Bandawe alisema mradi huo ambao umefikia kati ya asilimia 39 na 45, unajengwa na makandarasi tisa wakiwamo wa serikali na binafsi na umetoa ajira 2,149.

Kwa mujibu wa Bandawe, mradi huo unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 675 hadi kukamilika kwake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Udhibiti matukio ya mauaji upo umuhimu kupima afya ya akili

**MATUKIO** ya mauaji katika maeneo mbalimbali nchini yanaendelea kushamiri kila siku na yanayoripotiwa kwenye vyombo vya habari ni machache ambayo taarifa zake hutolewa na kupatikana polisi.

Takwimu zinaweza zisipatikane zote kutokana na matukio mengine kutoripotiwa kwa sababu mengine sio rahisi kuripotiwa kwa kuwa yanatokea bila watu wengine kujua.

Matukio mengi ya mauaji yanayoripotiwa sababu zinazotolewa ni kutokana na wivu wa mapenzi, mali, ushirikina na mambo mengine ya kifamilia.

Watu wanaofanya mauaji hayo wanatoka kwenye familia hizohizo, jambo ambalo linazua maswali mengi.

Jamii imekuwa ikijiuliza watu wamekuwa wanyama kiasi hicho na kwanini sasa matukio haya yanaendelea kushamiri kila siku pamoja na dola kutoa adhabu kali kwa wanaokutwa na makosa ya vitendo hivyo?

Wanasaikolojia mara nyingi wamekuwa wakitoa elimu ya dalili za watu ambao wanaonekana kuwa na utofauti wa maisha na wengine kufikia hatua ya kuchukua uamuzi huo wa mauaji.

Baadhi ya matukio ukiyafikiria unaweza ukashangaa kama aliyefanya alikuwa na akili timamu au kuna tatizo la afya ya akili.

Wengine huchukua uamuzi wa kujiua wenyewe kwa sababu zinazotolewa za ugumu wa maisha, msongo wa mawazo au kuchoshwa na magonjwa yanayomkabili.

Ndiyo maana wanasaikolojia wanatahadharisha jamii kuwa makini na watu wanaowaona kuwa na mabadiliko katika mienendo yao kama vile kujitenga na watu, kuwa mlevi wa kupindukia, mtu mwenye mawazo na wakati mwingine kutoa matamshi ya kutaka kujiua.

Katika baadhi ya matukio yaliyotokea hivi karibuni yanayohusu mauaji, ni tukio la binti aliyekutwa ameuawa na mwili wake kutupwa barabarani na watu wasiojulikana. Mwili wake pia ulikutwa pembeni ukiwa na chupa ya kilevi. Kwa nini ameuawa ni maswali ambayo wengi wanajiuliza.

Lakini, matukio yanayosikitisha zaidi ni ya ndugu wa karibu wakiwamo watoto kuua wazazi kwasababu ya kuwahisi ni wachawi au kutaka kurithishwa mali.

Tukio ambalo limeshangaza ndugu wa familia moja huko wilayani Masasi, mkoani Mtwara ni la mtoto kutuhumiwa kumuua baba yake mzazi kisa kikidaiwa kuwa aliwataka wamtafutie mchumba na alipoona ombi lake halijafanyiwa kazi akaamua kuchukua uamuzi huo wa kuondoa maisha ya mzazi wake mmoja huku akimwachia majeraha mama yake.

Ukijaribu kufikiria utaona kabisa hapa kuna tatizo la afya ya akili ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi kuanzia kwenye ngazi zetu za kifamilia.

Katika kipindi fulani kulikuwa na matukio ya kushamiri kwa ajali za bodaboda, lakini uchunguzi ulipofanyika ikabainika kuwa baadhi ya madereva wa vyombo hivyo hutembea na vilezi na kuvitumia wawapo kwenye shughuli zao.

Vivyo hivyo, kunahitajika ushirikiano wa hali ya juu wa kujichunguza katika familia zetu kuona umuhimu wa kuangalia afya zetu za akili ili matukio haya ya mauaji yaweze kudhibitiwa.

Jamii ndiyo yenye jicho la kwanza kumbaini mwenzake kutokana na mabadiliko atakayoyaona toka kwa mwanajamii mwenzake.

Kama taarifa itatolewa mapema na mtu huyo akachunguzwa na hata kumzungumza naye inaweza kusaidia kumwepusha na dhamira anayotaka kuichukua.

Wanajamii ni watu muhimu sana katika kutoa msaada kwa wenzao ili kunusuru janga kubwa lisiweze kutokea. Kwa pamoja tunaweza kudhibiti hali na pia maofisa Ustawi wa Jamii mnajukumu kubwa ni elimu ili kudhibiti vitendo hivi kuendelea kutokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wazazi, walezi msijisahau kukabili, kumaliza utoro

Na Sabato Kasika

**ELIMU** bora ni msingi mkuu wa maendeleo, kwani bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na ufahamu wa mazingira yanayomzunguka mwanadamu, inakuwa vigumu kuanzia familia hadi taifa kusonga mbele.

Kwa kawaida elimu ya msingi ni muhimu, kwa ajili ya kumjengea mwanafunzi msingi imara ambao utamwandaa kikamilifu hatimaye aweze kuendelea na ngazi za juu zaidi.

Hata hivyo, baadhi ya jamii ina mtazamo hasi kuhusu umuhimu wa elimu ya msingi, hali inayochangia kuwafanya baadhi ya wanafunzi kuwa watoro bila kuwachukulia hatua na hatimaye kuiacha shule.

Ninaamini kuwa, watoto wasipojengewa msingi wa kupenda elimu kuanzia ngazi ya chini, inaweza kuwa vigumu kupenda shule, hivyo ipo haja kwa wazazi na walezi kuhamasisha umuhimu wa elimu kwa watoto wao.

Katika mazingira hayo ya kutokuwa na mwamko na elimu, wapo baadhi ya wanafunzi wanadaiwa kuhudhuria vipindi vya masomo shuleni mara mbili, tatu kwa wiki, hali hiyo isipodhibitiwa inazaa utoro na hata kuacha shule.

Huenda ingekuwa ni vyema sasa kuunga mkono juhudi za serikali za kudhibiti utoro ziungwe mkono ili wote wapate elimu bila kuwapo na visingizio vya kutohudhuria shuleni.

Miongoni mwa sababu zinazochangia utoro, kukatisha masomo zinatajwa kuwa ni umaskini wa kipato kwenye familia, mimba za utotoni, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya jamii.

Ili kukabiliana na utoro wa wanafunzi wanaotoka familia maskini, Juni mwaka huu Waziri wa Fedha alipendekeza kuanzishwa kwa dirisha maalum kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), litakalosaidia watoto wanaotoka kwenye familia maskini.

Waziri anapendekeza kuanza utaratibu huo kwa kuwekeza Shilingi bilioni nane, kwa ajili ya watoto wa familia maskini watakaopatikana kwenye kanzidata ya TASAF na taarifa za wabunge na madiwani.

Hatua hiyo inachukuliwa kuonyesha ni jinsi gani elimu inapaswa kupewa kipaumbele kikubwa kama msingi imara wa kufikia malengo ya kuwa na taifa lenye wasomi na siyo wanaokwepa shule kwa visingizio mbalimbali.

Kutokana na mkakati huo, ni wazi kwamba kila mmoja wetu anahusika katika kudhibiti vitendo vya utoro ikiwamo kuanzia nyumbani kwa wazazi na walimu pia ili wanafunzi wote wahudhuria masomo.

Wapo wanafunzi ambao wanaweza kusingizia kuwa wanaumwa na kutohudhuria vipindi shuleni, na wakati mwingine ni ujanja tu na pia wapo wanaoaga kwenda shule na kuishia njiani.

Lakini katika mazingira hayo, kuna haja ya kuwapo ushirikiano kati ya wazazi na walimu, ili kupeana taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kama njia mojawapo ya kudhibiti vitendo vya utoro.

Ushirikiano huo kati ya wazazi na walimu ni mojawapo ya kudhibiti utoro, lakini iwapo wadau hao kila mmoja akidhani siyo wajibu wake kudhibiti vitendo hivyo, utoro utaendelea kuwapo nchini.

Serikali imeonyesha nia ya kutaka wanafunzi wote wapate elimu kwa kuondoa ada na pia imekuja na mkakati wa kusaidia familia maskini, hivyo ni wajibu wa wazazi na walezi kuhimiza watoto wao kupenda elimu.

Hatua hiyo ingeenda sambamba na kuwapo kwa chakula shuleni, watoto wao wapate angalau uji asubuhi na mlo wa mchana ili kupunguza utoro, unaolezwa kuwa unachangiwa na ukosefu wa chakula shuleni.

Pamoja na hayo, ninadhani michezo, muziki na stadi za kazi vingepewa kipaumbele kama njia ya kuvutia wanafunzi kupenda shule, kwani navyo vina sehemu yake hasa kukuza vipaji.

# Halmashauri zaonywa kushindwa kuhuisha mikataba vituo binafsi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amezionya halmashauri zinazoshindwa kuhuisha mikataba ya vituo vya afya vya taasisi za dini, hali inayosababisha kukosa uhusiano mzuri.

Bashungwa alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mkutano wa 85 wa Chama cha Madaktari wa Hospitali za Mashirika ya Dini (TCMA).

Alisema hataki kusikia kuna mawasiliano na mahusiano hafifu kati ya waganga wakuu wa mikoa, wakurugenzi wa halmashauri na taasisi za dini ambazo zinatoa huduma za afya kwa wananchi.

"Namwagiza Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, sitaki kuendelea kusikia mawasiliano hafifu kati ya waganga wakuu wa mikoa, wakurugenzi na taasisi za dini ambazo zinatoa huduma kwa wananchi. Ni lazima tuboreshe uhusiano. Mimi Waziri wa Nchi TAMISEMI kwa kuheshimu majukumu ambayo TCMA mnayafanya kwa kushirikiana na serikali, nimeacha majukumu ili kuangalia jambo linaenda vizuri," alisema.

"Sasa ni mkurugenzi gani wa halmashauri gani na ni mganga mkuu gani wa wilaya atakayepuuzia hili. Kwa kweli atakuwa hiyo kazi haitaki. Mara moja tuanzie hapo lakini sasa tuipe timu mapitio hayo ya mikataba waipitishe ili tukubaliane jinsi ya kulitekeleza," alisisitiza.

Awali, Rais wa TCMA, Dk. Paul Kisanga, alisema baadhi ya halmashauri zimekuwa zikishindwa kuhuisha mikataba ya vituo vya afya vya kanisa hata pale ambapo bado kituo cha serikali hakijafikia kutoa huduma stahiki kwa wagonjwa.

Pia alisema lengo la mkutano huo ni kujadili jinsi ya kuboresha huduma za afya na kukuza ushirikiano kati ya madaktari na watoa huduma pamoja na kubadilishana mawazo kutafuta njia za kutatua matatizo ya utoaji wa huduma.

Alisema hospitali nyingi za makanisa ziko katika maeneo ya vijijini ambako ndiko waliko wananchi wengi na watu wenye uwezo mdogo wa kumudu hali ya maisha.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kikristo ya Huduma za Kijamii (CSSC), Peter Maduki, alimhakikishia Waziri Bashungwa kuwa wataendelea kufanya kazi na serikali ili kutoa huduma bora kwa wananchi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa majengo ya wizara mbalimbali katika Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Wavuvi wamtwisha Kinana zigo la kero

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, amepokea malalamiko 13 ya wavuvi wa samaki katika Ziwa Victoria ikiwamo utitiri wa kodi na mateso wanayoyapata wanapokuwa ziwani.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Kinana ameahidi kuyafikisha katika mamkala husika ili kupatiwa ufumbuzi.

Pia amesema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kutatua changamoto mbalimbali zikiwamo za kisheria, hivyo zilizotolewa na wavuvi zitafanyiwa kazi ili kuifanya sekta ya uvuvi kuwa na tija zaidi.

Kinana ameyasema hayo jana jijini Mwanza alipozungumza na wavuvi wa Ziwa Victoria katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), akiwa katika ziara ya kukagua uhai wa chama na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

"Ndugu zangu nimekuja hapa kuwasikiliza kwa sababu mbili, kwanza, serikali hii ni ya CCM na pili nimekuja kuwasikiliza. Nimewasikiliza vizuri na kwa umakini, nimesikiliza risala pamoja na wasemaji wengine na yote yaliyozungumzwa na mliyosema tumeandika.

"Rais lengo lake kuu ni kuwasaidia Watanzania ili kipato chao kiendelee kuongezeka wanapofanya biashara. Tunapozungumzia sekta binafsi imara nyingi tunawafikiria wawekezaji wakubwa wa viwanda na wakati mwingine tunawafikiria hata watu kutoka nje pekee.

"Ieleweke ukiifikiria sekta binafsi ni hawa (wajasiriamali wadogo) na ndio wenye viwanda vidogo. Wanajituma ili wawe na maisha bora. Serikali haiwezi kumwondolea mtu umaskini wake, lakini inaweza kutengeneza mazingira mazuri, sheria na kanuni nzuri ili iwe rahisi kwa mtu kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kwa faida. Hiyo ndiyo kazi ya serikali," alisema Kinana.

Aliongeza kuwa wakati anasikiliza risala ya wavuvi, miongoni mwa malalamiko ni uwapo wa kodi 11 ambazo ili kumudu lazima uwe na kipato kikubwa huku akieleza kushangazwa na uwepo wa kodi ya maegesho ya vyombo vya uvuvi. "Imenifanya nicheke eti kuna kodi ya 'parking' yaani kodi zote wamechukua mwisho wa siku wamekuja na parking. Sasa hivi kodi nyingi kidogo, natolea mfano tu, lakini niwaambie nia ya Rais na nimemsikia amezungumza juu ya malengo manne aliyo nayo maana la kwanza ni kuleta maridhiano kwa Watanzania, kuleta maboresho ya serikali katika muundo, sheria, sera na kanuni ili maisha ya watu yawe bora zaidi.

"Sasa katika kuboresha mambo risala yenu hii itatizamwa namna gani tunaweza kubadili mambo yao yawe bora zaidi. Risala yenu itatazamwa namna gani tunaweza kubadilisha mambo ambayo yapo kama 14," alisema.

Pia alisema baada ya miaka mingi Rais Samia ametoa fedha za ruzuku kwa ajili ya wakulima, lakini ametoa fedha za ruzuku kwa baadhi ya wavuvi ambapo ametoa fedha kwa ajili ya kutengeneza viamba na kwa mkoa wa Mwanza umepata viamba 42. "Kwa hiyo Rais ana lengo zuri, anaweza kuwa na nia njema, malengo mazuri lakini Watanzania lazima tumsaidie ili kazi na malengo yaweze kufikiwa. Risala yenu hii ni moja ya njia ya kumsaidia Rais Samia kuwasaidia Watanzania kuondokana na umaskini vile vile kuwa matajiri kupitia uvuvi,"alisema Kinana.

Hivyo amewaahidi kupitia nafasi aliyo nayo vikao alivyo navyo kwa namna anachohusika na chama na serikali yake hayo mambo yote waliyoyasema yatashughulikiwa ipasavyo.

"Sina jibu la kutoa hapa na si vizuri nikaanza kuyajibu haya mambo kwasababu mliniita niwasilikize, nimewasikiliza mmeniomba na kunitaka kama Chama kinachounda serikali yake kitafute namna ya kutatua matatizo haya.

"Niwaahidi nitakwenda kuwahakikisha haya masuala yote yaliyotolewa humu ndani yanapata majibu na yanapata ufumbuzi. Yako yanayohusu serikali ya utekelezaji, wizara, sera, sheria pamoja na kanuni zinazotungwa na serikali hasa wizara. Nitatizama namna gani nitasaidia ili na ninyi kwa yale mliyoyasema yaweze kufanikiwa," alisema Kinana.

Awali akisoma risala ya wavuvi, Katibu wa Kamati ya Ushauri wa Wavuvi Ziwa Victoria Mayalu Kasiri, alielezea changamoto na matatizo yanayosumbua sekta ya uvuvi na kusababisha kudorora.

Alitaja changamoto hizo kuwa ni kukithiri kwa uvuvi haramu ambalo limekuwa likiitesa sekta hiyo katika Ziwa Victoria, pili biashara holela ya mabondo ya Sangara ambayo inachangia uwepo wa uvuvi haramu, uvamizi, utekaji na unyang'anyi wa samaki kwa wavuvi ziwani.

"Tunaomba serikali kuweka mfumo rasmi wa wavuvi kwani kumekuwa na matatizo mengi ya wavuvi kuhusu kukosa mitaji ni zana bora za uvuvi, hivyo tunaomba serikali yetu kuweka mfuko maalumu kwa ajili ya wavuvi tu kuliko ilivyo sasa kupitia benki ya kilimo ambayo mvuvi akienda hakopeshiki mpaka alete dhamana ya mali zao kama hati ya nyumba," amesema.

Ametaja changamoto nyingine ni tozo ya ushuru wa wavuvi ambazo ziko 11 na ambapo meeleza kwa muda mrefu sasa wamekuwa na utitiri wa tozo na ushuru ambazo hulipwa na wavuvi na kufanya wabebe mzigo mzito na hatimaye washindwe kujikwamua dhidi ya umaskini.

Changamoto nyingine, alisema ni ulinzi na usalama wa mali za wavuvi kwani kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakipatwa na majanga pindi wawapo katika kazi za ziwani. Pia alisema mafuta kwa ajili ya wavuvi ambayo wamekuwa wakitumia ni petroli, dizeli na mafuta ya taa ambayo bei yake kwa sasa iko juu.

Pia alisema sheria za uvuvi na kanuni zake zilizopo sasa ni kandamizi kwa wavuvi kwani hazitoi mwanya wa mvuvi kupata haki zake kama raia wa Tanzania. Wakati nyingine ni bei kubwa ya zana za uvuvi.

**•Imeandikwa na Beatrice Shayo na Richard Makore, MWANZA**

# Wamiliki haramu silaha waonywa

**Na Magdalena Jackson (SJMC)**

SERIKALI imesema bado kuna baadhi ya watu wanaomiliki silaha zilizokuwa zikimilikiwa kihalali na ndugu zao waliofariki dunia badala ya kuzisalimisha katika vituo vya polisi.

Kutokana na hali hiyo, imetoa wito kwa kundi hilo kusalimisha silaha hizo kwa kuwa kuendelea kubaki nazo ni makosa zinaweza kuhatarisha usalama wa raia na mali zao.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alisema hayo jana wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa Mwezi wa Msamaha wa Afrika, kusalimisha silaha haramu uliofanyika katika viwanja vya Mashujaa jijini Dodoma.

Sagini alisema mtu yeyote atakayesalimisha kwa hiari silaha anayoimiliki kinyume cha sheria hatoshtakiwa.

"Kuna wengine wanamiliki silaha kihalali lakini wanaona hakuna ulazima wa kumiliki silaha hizo na wengine. Afya zao au umri wao haviwawezeshi kuendelea kumiliki silaha, hivyo nawaombwa wazisalimishe silaha hizo ili zisiingie katika mikono isiyo salama," alisema.

Sagini alitumia fursa hiyo kuviomba vyombo vya habari kushirikiana na Jeshi la Polisi kuhamasisha umma wa Watanzania kujitokeza kwa wingi na kusalimisha silaha haramu kwa kipindi kilichotolewa.

Alisema silaha haramu zinachangia kwa kiasi kikubwa kuvuruga amani ya nchi na kudhoofisha demokrasia na uhuru wa wananchi.

"Hivyo tunavyozindua kampeni hii tunapeleka ujumbe kuwa serikali inataka kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania wanaishi na kutekeleza kazi mbalimbali kwa amani.

"Nawataka wakuu wa mikoa na wilaya nchini kwa kusaidiana na makamanda wa polisi wa mikoa kuongoza mpango wa uhamasishaji wananchi katika kampeni hii," alisisitiza.

Sagini, alisema usalimishaji huo ulianza Septemba Mosi na unatarajiwa kuhitimishwa Oktoba 31, mwaka huu, na iwapo mtu atakutwa na silaha haramu baada ya muda huo atachukuliwa hatua kama wahalifu wengine kwa sababu atakuwa ameshindwa kutekeleza matakwa ya msamaha huo.

"Kampeni hii ni fursa ya kuonesha mwendelezo wa dhamira ya nchi katika masuala ya amani na usalama barani Afrika. Kwa sasa Tanzania ni mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika," alisema.

Pia aliwataka wamiliki wa silaha kwa halali lakini wanaona hakuna ulazima wa kumiliki au afya zao na umri hauruhusu kuhimili matumizi ya silaha wasalimishe silaha hizo ili zisiingie katika mikono isiyosalama.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alisema Tanzania ilitia saini mikataba mbalimbali yakiwamo makubaliano ya Umoja wa Afrika wa kuondosha silaha haramu na kutangaza Septemba kuwa mwezi wa kusalimisha silaha hizo kuanzia mwaka 2017 hadi 2030.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, Januari 2019 hadi Juni, 2022 silaha 997 zilikamatwa katika operesheni mbalimbali za kuzuia na kutanzua uhalifu na wahalifu. Kati ya hizo 52 zilikuwa zinamilikiwa kihalali lakini ziliibiwa kutoka kwa wamiliki hao," alisema.



Meneja wa Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia (TAZARA), Fuad Abdalla, akitoa majibu ya maswali yaliyoulizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utendaji wa mamlaka hiyo baada ya kuwasilisha taarifa yao kwa kamati jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Makamba amwakilisha Rais Mkutano wa Dunia Mabadiliko Tabianchi Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye Mkutano wa Viongozi wa Dunia unaojadili Programu ya Afrika ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa Adaptation Summit) unaofanyika Rotterdam, Uholanzi.

Mkutano huo ulioanza jana, unalenga kushawishi washirika wa maendeleo, taasisi za kifedha na sekta binafsi na marafiki wa Afrika kuchangia fedha kwenye programu hiyo ambayo inahitaji Dola za Marekani Bilioni 25 ifikapo 2025.

Katika kufanikisha azma hiyo, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imechangia Dola za Marekani bilioni 12.5.

Mkutano huu unafanyika kama sehemu ya maandalizi ya mkutano wa 27 nchi wanachama wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi ambao unatarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu, Sharm El Sheik, Misri ambako suala la kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa Afrika ni moja ya agenda muhimu.

Katika mkutano huo, Waziri Makamba alikutana na viongozi wa dunia, wakuu wa taasisi na mashirika mbalimbali na kujadiliana nao fursa mbalimbali ikiwamo namna bora ya Tanzania kunufaika na mpango huo wa 'Africa Adaptation Acceleration Program' (AAAP) ambao utaharakisha mipango ya nchi katika kukabiliana na majanga yakiwamo UVIKO - 19, ukame, njaa, ajira kwa vijana na mafuriko.

Mkutano huo uliongozwa na Rais wa Senegal na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), Macky Sally, na Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa (UN), Ban Ki-Moon ambaye ni Mwenyekiti wa Kituo cha Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (GCA).

# WFP kutumia fedha za Japan kununua mazao kwa wakulima

**Na Faustine Feliciane**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limepokea msaada wa Dola za Marekani 500,000 (zaidi ya Sh. bilioni 1.1) zitakazotumika kununua mazao kwa wakulima wa ndani.

Mazao hayo ni kwa ajili ya chakula cha wakimbizi kutoka Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo walioko kwenye kambi zilizoko Kigoma. Kambi hizo ni Nyarugusu na Nduta ambazo zina wakimbizi 204,000.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya makabidhiano ya msaada huo nyumbani kwa Balozi wa Japan nchini Tanzania, Yasushi Misawa, Mkurugenzi na Mwakilishi wa WFP Tanzania, Sarah Gordon- Gibson, alisema WFP inaishukuru Japan kwa mchango huo uliotolewa ambao umetolewa kwa wakati unaofaa.

"Msaada huu kutoka Japan utasaidia kwa kiasi kikubwa kuwekeza katika uchumi wa Tanzania kupitia ununuzi wa ndani wa maharage ambao hatimaye utazifikia kwa haraka kaya za wakimbizi walio katika mazingira magumu," alisema.

Alisema, serikali ya Japan imekuwa ikitoa msaada wa chakula cha binadamu kwa nchi zinazoendelea tangu mwaka 1968 na ni mshirika wa muda mrefu wa WFP nchini Tanzania.

"Fedha hizi zitatumika kununua tani 260 za maharage kwa ajili ya kikapu cha chakula cha WFP ambacho kina nafaka, mchanganyiko wa ngano iliyoongezewa nguvu, soya na sukari, kunde, mafuta ya kula na chumvi.

Tunaishukuru sana Japan," alisema. Mkurugenzi huyo alisema wakulima wa Tanzania watapata fursa na uhakika wa kuuza mazao yao hususani maharage na mengine yaliyotajwa.

Alisema, uhaba mkubwa wa fedha katika miaka ya hivi karibuni, umeilazimu WFP kupunguza mgawo kwa wakimbizi katika kambi za Nyarugusu na Nduta, wakati mwingine hadi theluthi mbili ya mahitaji yao ya chini ya kalori za kila siku, jambo ambalo lina athari mbaya kwa afya na ustawi wa wakimbizi.

Balozi Misawa, kwa upande wake alisema Japan itaendelea kuunga mkono juhudi za WFP katika kuwasaidia wakimbizi walioko kwenye kambi.

"Japan ni muungaji mkono mkubwa wa WFP duniani kote, na inashukuru kwa jukumu la shirika hilo katika kukabiliana na mahitaji ya watu walio katika mazingira magumu, hivyo ninafurahi kutoa mchango huu kwa niaba ya serikali na watu wa Japan kwa Tanzania, nikijua kwamba utasaidia kukidhi mahitaji ya dharura ya chakula kwa watu walio katika mazingira magumu," alisema.

## Waandishi wahimizwa utatuzi wa migogoro jamii

**Na Beatrice Moses,** DODOMA

MIGOGORO kadhaa inayoibuka kwenye jamii nchini ikiwamo inayohusu umilikishwaji wa mali kutokana na wosia, inaweza kuzuilika iwapo sheria na katiba zitazingatiwa katika ngazi zote.

Waandishi wa habari wanawake, wametajwa kuwa ni miongoni mwa watu wanaoweza kusaidia jamii kuepukana na migogoro hiyo kwa kuibua na kuandika habari zinazoonyesha umuhimu wa sheria na kuzingatiwa pamoja na jamii kuitambua Katiba ya nchi na mwongozo wake kwa wananchi na watawala.

Meneja Programu wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Mackphason Mshana, alisema juzi kwamba wosia ulioandaliwa kwa kuzingatia sheria ni suluhisho la migogoro ya mirathi, inapotokea umeandikwa kwa makosa huwa sababu ya kuchochea migogoro.

"Wosia ni siri haupaswi kujulikana hadi inapotokea mhusika amefariki dunia. Hapo unapaswa kujulikana aliacha maagizo gani katika mgawanyo wa mali zake lakini ukijulikana mapema unakuwa batili. "Pia unaweza kusababisha mambo mabaya ikiwamo kuuawa kwa mhusika, hivyo wanahabari mnalo jukumu la kuelimisha jamii itambue jambo hili," alisema Mshana kwenye mafunzo maalumu ya siku mbili ya kuwajengea uwezo wa kuandika habari kwa kuhusisha Sera na Sheria waandishi wa habari wanawake 28 kutoka Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) yaliyoandaliwa na TLS.

Mwezeshaji katika mafunzo hayo, Wakili Mary Mwita kutoka TLS, ambaye pia ni mwandishi wa habari mwandamizi, alielezea jinsi gani waandishi wanapaswa kuifanya jamii itambue katika Utawala wa kidemokrasia ulivyo muhimu kwa maendeleo ya nyanja mbalimbali.

"Wanahabari mna jukumu la kuielezea jamii umuhimu wa utawala wa kidemokrasia, kuchunguza mikataba kandamizi, matumizi ya madaraka yanayozingatia sheria na Katiba. Pia andikeni sheria na sera zipi zinazokosekana zinasababisha watu kupata usumbufu mfano sheria ya wazee," alisema.

Kuanzia kwenye ngazi ya kaya, viongozi wa mitaa, vijiji hadi taifa wanapaswa kuhakikisha wanazingatia mwongozo unaotolewa kwenye katiba pamoja na kuzingatia sheria zilizoko.

Rais wa UTPC, Deo Nsokolo, akizungumza awali katika ufunguzi wa mafunzo hayo, aliishukuru TLS, kwa ushirikiano mzuri na wanahabari ambao ni wazi utainufaisha jamii kwa kuwa itaongeza kuibuliwa kwa habari mbalimbali zilizopo kwenye jamii ambazo zinahusisha utatuzi wake kisheria.

# TGGA yanoa wasichana kukabiliana athari za mabadiliko ya tabia nchi

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Kujitolea cha Maskauti wa Kike Tanzania (TGGA), chini ya mwavuli wa World Association of Girls Guides and Girls Scout (WAGGGS) kimetoa mafunzo ya namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wasichana 20 kutoka mikoa 12 ya Tanzania bara na visiwani ili wakalete mabadiliko katika jamii zao.

Akizungumza katika hafla ya kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku tatu, Meneja Mradi wa chama hicho taifa, Nyendo Kinyonga, alisema mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wasichana hao ili wakawe mawakala wa utetezi wa athari za mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo wanayotoka.

Nyendo alisema mradi uligawanyika katika maeneo matatu ambayo ni kufundisha kuhusu athari hizo, kutekeleza kwa vitendo mafunzo waliyopewa pamoja na jinsi ya kuwafikia na kuwasiliana na watoa uamuzi.

"Tunategemea baada ya mafunzo haya jamii itakuwa na uelewa mkubwa juu ya athari za mabadiliko ya tabia nchi na namna ya kukabiliana nao kupitia elimu itakayotolewa ma wasichana hawa," alisema.

Alisema wametoa mafunzo hayo kwa wasichana kwa sababu ndio kundi linaloathirika zaidi na athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa sababu ya jukumu kubwa la walionalo la kuhudumia jamii.

"Kunapokuwa na shida ya maji, mwanamke ndiye anayetembea umbali mrefu kuyatafuta ili apeleke nyumbani. Huko wanakumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo kubakwa, kwa hiyo tumewapa mafunzo haya ili wakawe mstari wa kuleta suluhisho za changamoto zinazowakabili," alisema.

Naye Meneja wa Uchechemuzi Mradi huo kutoka WAGGGS, Germaine Umuraza, alisema wamechagua kupeleka mradi huo Tanzania kutokana na Ripoti ya Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi ya Shirika la Kimataifa la Mazingira (UNEP) kuonyesha wanawake wa nchi hiyo kuwa katika hatari ya athari za mabadiliko hayo.

"Tunategemea wasichana wakalete mabadiliko katika jamii zao kwa kuwaelimisha namna wanavyoweza kuafanya kuleta uhimilivu wa athari hizo, lakini pia namna nzuri ya kuwasiliana na watoa maamuzi ili katika kuleta mabadiliko hayo," alisema.

Mmoja wa wasichana waliopatiwa mafunzo hayo kutoka Mkoa wa Shinyanga, Joyce Maganga, alisema atakwenda kuelimisha jamii yake kuhusu uhusiano uliopo kati ya kukata miti na athari za mabadiliko ya tabia nchi ili kuikomesha tabia hiyo.

Alisema pia atahamasisha viongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi mkoa kutumia sheria na kanuni zilizotungwa ili kupambana na janga la ukataji miti lililoshamiri katika mkoa huo.

"Ninatamani kuona sheria zilizotungwa za kuzuia ukataji wa miti, zitiliwe mkazo katika mkoa wetu kwa sababu nako kuna uharibifu mkubwa unaotokana na shughuli za kutengeneza mkaa," alisema.



Mtendaji Mkuu wa Kampuni za Huduma za Meli (MSL), Eric Hamiss, akimwelezea Makamu Mwenyekiti wa CCM, Abdulrahman Kinana, jana alipokuwa akitembelea Bandari ya Mwanza Kusini ikiwa ni ziara ya siku mbili. **PICHA: ROSE JACOB**

# Kampuni yaingiza vitabu 500,000 kuchochea kasi usomaji wa vitabu

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Big Bad Wolf, ambayo inajulikana kwa uuzaji wa vitabu duniani, imeingiza nchini vitabu 500,000 ikiwa ni mwendelezo wa jitihada za kujenga kizazi kipya cha wasomaji wa vitabu.

Vitabu hivyo vinatarajiwa kuonyeshwa kwenye ufunguzi utakaofanyika kwenye ukumbi wa Diamond Jubelee, jijini Dar es Salaam, kuanzia keshokutwa hadi Septemba 18, mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mwanzilishi Mwenza wa Big Bad Wolf, Andrew Yap, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Big Bad Wolf Sharjah, akiwa na mwakilishi wa Tanzania, Mohamed Noor Hers.

Alisema, kuingia kwenye maonyesho hayo itakuwa bure na kwamba kwa watakaotaka kununua vitabu hivyo uuzaji utakuwa wazi kwa umma kila siku kwa siku zote 10 watakazokuwa kwenye ukumbi huo.

Alisema walifurahishwa na kupendezwa kuleta mauzo ya vitabu nchini Tanzania kwa mara ya kwanza baada ya kuona kuna soko kubwa na wepesi wa kuingia.

"Kwa hakika ni hatua ya kusisimua na muhimu kwetu katika vitabu vya Big Bad Wolf tuliposafiri kuelekea Afrika, na kuja Tanzania kama kimbilio letu la kwanza. Dhamira yetu kuu siku zote imekuwa kukuza mazoea ya kusoma Kiingereza duniani kote na kujenga kizazi kipya cha wasomaji kwa kufanya vitabu kuwa bei nafuu na kupatikana kwa kila mtu," alisema.

"Pamoja na mada 15,000 zinazopatikana na vitabu 500,000 vipya vya Kiingereza vinavyotolewa, tunataka Watanzania kutoka nyanja mbalimbali wawe vijana au wazee, wagundue furaha ya kusoma na kupata maarifa, bila kujali kiwango cha mapato yao," aliongeza.

Alisema, ni matumaini yao kuwa Watanzania watafaidika kwa kiasi kikubwa na uuzaji wa vitabu hivyo vilivyosheheni maarifa mengi na kuwataka watanzania kutembelea maonyesho hayo kujionea aina mbalimbali ya vitabu walivyoleta.

Kwenye vitabu hivyo, alisema kuna riwaya zinazouzwa sana, hadithi za sayansi, mapenzi, fasihi na riwaya za michoro hadi vitabu vya biashara, binafsi, msaada, vitabu vya usanifu, vitabu vya kupikia na mengi zaidi.

Alisema, kuna vitabu vya watoto ikijumuisha vitabu vya picha, vitabu vya shughuli, vitabu vya kupaka rangi na vitabu shiriki vya masomo.

Vitabu vya Big Bad Wolf, alisema vilizinduliwa Kuala Lumpur, Malaysia, mwaka 2009 na dhamira ya waanzilishi ni kukuza tabia ya kusoma, kuongeza ujuzi wa kusoma Kiingereza ulimwenguni kote.

Alitaja lengo lingine kuwa ni kujenga kizazi kipya cha wasomaji kwa kufanya vitabu kuwa vya bei nafuu na kufikiwa na kila mtu.

"Uuzaji huu ni mpango wa kimataifa ambao unalenga kuhimiza watu wa kila rika kugundua furaha ya kusoma, kuwatia moyo kutimiza ndoto zao na muhimu zaidi kuwawezesha na maarifa ya kuzitimiza ndoto zao," alisema. Alisema, wanaamini kwamba kadri mtu anavyopata ujuzi mwingi ndivyo anavyoweza kukidhi matakwa ya ulimwengu wa leo yenye ushindani.

Tangu kuanzishwa kwake, alisema uuzaji wa vitabu vya Big Bad Wolf, umebadilisha maisha ya watu wengi kwenye nchi za Kambodia, HongKong, Indonesia, Myanmar, Pakistan, Ufilipino, Singapore, Sri Lanka, Korea Kusini, Thailand, Taiwan, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) pamoja na Malaysia.

# KCB yapigia debe wanawake kushika nafasi za juu uongozi

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kuongeza idadi ya wanawake wanaoshika nafasi za ngazi za juu katika uongozi, Benki ya KCB Tanzania imejipanga kuwawezesha wanawake kupata mafunzo ya uongozi.

Benki hiyo imesema, utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa taasisi zinazoongozwa na wanawake zinakuwa katika nafasi ya kutengeneza faida zaidi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa KCB Tanzania, Cosmas Kimario, katika mahafali ya pili ya mpango wa kuendeleza viongozi wa kada ya juu katika taasisi za umma na binafsi unaofanyika chini ya Umoja wa Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni Binafsi nchini (CEOrt).

Alisema, wanaamini ili mtu kupata mafanikio lazima kuwekeza katika uongozi na kwamba wameweka kipaumbele katika jinsia kwa sababu wanataka kupata viongozi wengi wanawake.

"Tunataka tupate viongozi wengi hasa wanawake, tuweke wanawake wengi viongozi kwa sababu tumeona faida zake, tumeanza na huyu mmoja lakini katika hatua zijazo tutaendelea kuweka wengine," alisema.

Kimario, alisema uongozi unahitaji mtu mwenye ujuzi wa kushughulika na watu pia kuwa kiongozi ambaye anakataza vitu ambavyo yeye hafanyi.

"Huwezi kuwa kiongozi ambaye unawaambia wenzako wahini kazini wakati wewe unakuja kazini saa tano, ndiyo maana tunataka tuwafundishe viongozi wetu wafundishwe si lazima wawe wakurugenzi lakini wawe viongozi bora kwa wale wanaowaongoza," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wanaamini mtu akipitia mafunzo ya uongozi anabadilishana na wengine ujuzi huo waliopo ofisini na mwisho ufanisi wake unaonekana.

Naye, Antonia Kilama, ambaye ni Mkuu wa Idara ya Sheria na Katibu wa Benki hiyo, alisema mafunzo hayo yamemuelimisha kuhusu kuwaelewa wafanyabiashara na kuikumbusha benki namna ya kufuata sheria.

"Siyo tunaweka sheria mbele lazima tufuate sheria na tuwasaidie wateja wetu katika mfumo ambao ni rahisi na haraka zaidi, kitu kikubwa ni wateja wetu tunawasaidia nini," alisema

Alisema pia, wamefundishwa namna ya kuwapa watu nafasi waliopo chini yake ili waweze kukua na kutoka sehemu iliyopo.

"Unaanza kwangu lakini unaweza kushauri benki ni namna gani tunaweza kutumia ili tuweze kuwafikia watu wengi zaidi," alisema Antonia.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango (Sera), Lawrence Mafuru, alisema mpango wa kuwaandaa viongozi vijana kwa ajili ya kushika nafasi za juu umelenga kujibu kiu ya watu wengi ikiwemo wawekezaji wanapokuja Tanzania na kuhitaji wasimamizi wa taasisi zao.



Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa Benki ya NCBA, Genesi Kunda (wa pili kulia), akiwakabidhi washindi watatu zawadi za kila wiki ya pikipiki katika viwanja vya soko la Mabibo katika kampeni ya Mpawa inayohamasisha wateja kuweka akiba, kukopa na kurejesha mikopo mapema ili kujishindia zawadi bora za kila wiki na kampeni ijulikanayo 'Chuzi Limekubali' kwa kushirikiana na kampuni ya simu ya Vodacom. Wa kwanza kushoto ni Jackson Maka akipokea zawadi kwa niaba ya Salome Kapela, akifuatiwa na Ibrahim Nzunda, Annastazia Yenze (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kutumia mitandao kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Morogoro wamesisitizwa kutumia fursa za mtandaoni kujinufaisha katika kukuza shughuli zao za kilimo, ujasiriamali, elimu na ukuzaji tija katika maendeleo binafsi na ya taifa.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Mawasiliano wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Robin Ulikaye, wakati akitoa elimu kwa wananchi waliofika kujipatia mahitaji mbalimbali katika soko la mnada wa Jumapili ambalo hufanyika kila Jumapili eneo la mjini hapa.

Alisema TCRA ilifika kwenye soko hilo la mnada kuwapa wananchi elimu juu ya matumizi ya huduma za mawasiliano ikiwamo fursa zinazopatikana katika anga la kimtandao "the cyber space".

Ulikaye aliwaeleza wananchi kuwa TCRA kupitia kampeni yao ya Kwea Kidijitali, inalenga kuhakikisha wananchi wote wanapata elimu stahiki ya matumizi sahihi na salama ya mtandao, ikiwa ni pamoja na kung'amua fursa zilizomo kwenye anga la kimtandao.

"Mitandao ina fursa nyingi zikiwamo kupata elimu kwa wanafunzi, kujifunza na kupata masoko ya shughuli zako za ujasiriamali, kilimo, biashara na nyingine nyingi zinazokuwezesha kukwea kidijitali. TCRA tunasisitiza unapotumia mitandao hiyo hakikisha umehakiki usajili wa laini zako za simu kwa kubofya *106#, kisha ufuate maelekezo," alisisitiza Ulikaye.

Alibainisha kuwa mtu anapobaini namba asiyoifahamu fika kwa mtoa huduma wake kuiondoa mara moja. Aidha, alisisitiza kuwa kutoa taarifa kwa kikosi kazi kinachohusisha Jeshi la Polisi, mtumiaji wa huduma za mawasiliano anapopokea ujumbe wa kitapeli, anapaswa kuripoti namba iliyomtumia ujumbe huo kwenda namba 15040, huduma aliyosisitiza kuwa haitozwi gharama zozote kwa mtumiaji wa huduma anayetoa taarifa.

Ofisa huyo alisema katika kazi hiyo ya kuwaelimisha wananchi kuhusu Mawasiliano TCRA iliambatana na watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu pamoja na Jeshi la Polisi, kwa shabaha ya kuwapatia wananchi wa Morogoro huduma zilizokamilika kuhusu mawasiliano.

Akizungumzia ushiriki wa Jeshi la Polisi kwenye kampeni hiyo, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi ambaye anasimamia Kitengo cha Mitandao, Fadhili Magombela, alibainisha lengo la jeshi hilo kuhakikisha wananchi wanapata elimu kwa kina kuhusu usalama wao wanapokuwa kwenye anga la mtandao.

"Maisha kwenye mtandao hayatofautiani sana na maisha katika ulimwengu wa kawaida, kwa hiyo tunapenda kuwasisitiza wananchi, wakati wote kuhakikisha wanakuwa makini wanapokuwa kwenye mazingira ya kimtandao kwa kuwa uhalifu huko ni halisi.

Aidha, tunawaasa wananchi ukitapeliwa au kunusurika katika utapeli mtandaoni hakikisha unatoa taarifa katika kituo cha polisi jirani yako ili hatua zichukuliwe," alisema.

## Wapewa mafunzo kushiriki uongozi

**Na Sabato Kasika**

BAADHI ya wanawake katika kata za Majohe na Kipunguni jijini Dar es Salaam, wameanza kupata mafunzo kwa vitendo ili kuwajengea uwezo wa kupata ujasiri wa kushiriki katika shughuli za kisiasa bila woga.

Mafunzo hayo yanatolewa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, ikiwa ni njia mojawapo ambayo itachangia kuhakikisha idadi ya wanawake inaongezeka kwenye nafasi ya maamuzi.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Seleman Bishagazi, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili juzi, wakati wa mafunzo na kufafanua kuwa yalianza tangu mwezi uliopita na yataendelea hadi Desemba mwaka huu.

"Kwa kawaida, mashirika mengi hutoa mafunzo ya uongozi kwa wanawake darasani tu, sisi tunafanya kwa vitendo, katika kata mbili za Majohe na Kipunguni ili wanawake wawe na mwamko," alisema.

Bishagazi alisema kituo chake kimegundua kuwa wanawake wengi huwa hawana ujasiri wa kusimama kwenye majukwaa kuomba kura, hivyo kituo hicho kikaamua kuainisha mafunzo hayo kwa vitendo.

"Women Fund Tanzania (WFT) wamefadhili mafunzo haya na tumeona tuanzie huku kwetu, ili tuwajengee uwezo wa kujiamini kwa kipindi cha miezi sita, waweze kusimama bila woga na kujinadi kwa wananchi wakati wa kampeni iwapo watajitokeza kuwania uongozi mwaka 2024 na 2025," alisema.

Alifafanua kuwa katika kampeni, wakati mwingine huwa kuna maswali na kwamba kituo hicho kinawaandalia mfano wa mikutano ya kampeni na kuwasimamisha wajinadi huku wakiulizwa maswali.

"Wanajinadi na kuomba kura na kuulizwa maswali na kuyajibu, huku sisi wasimamizi wa mafunzo tukisahihisha kasoro tunazoziona pale pale kwenye mafunzo," alisema.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mariam Ngomaitara, alisema yatawasaidia kujiamini na kuwa na ujasiri wa kukabiliana na rushwa ya ngono katika uchaguzi.

"Wengi tunataka uongozi, ila huwa tunakwamishwa na kutojiamini na pia suala la rushwa ya ngono, lakini mafunzo hayo yanatupa ujasiri wa kukabiliana na yote hayo," alisema.

Mshiriki mwingine, Livia Mhagama, alisema ipo haja wafadhili kuangalia uwezekano wa kuwezesha wadau kama Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni ili wanawake wote nchini wapate mafunzo hayo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 6, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## Wahadzabe 'wafalme wa msituni' waliobobea kulinda kila kiumbe


Ukurasa 12


Ukurasa 13

Una maoni kuhusu ubunifu, teknolojia?

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Aliyetibuliwa mpango wa kuozwa asimulia mwanzo, mwisho mambo yalivyokuwa

•Wazazi mkoa anakotoka waaswa 'tafakarini njia zenu'


Mwanafunzi aliyelazimishwa kuozwa (jina linahifadhiwa) (kushoto), akielezea namna alivyotaka kuozeshwa kwa mahari ya ng'ombe 10 na Sh. 200,000. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

WAKAZI wa Kijiji cha Manyada kilichoko wilayani Shinyanga, Agosti 16 walijipanga 'kuupiga mwingi, kula mpunga' na kusherehekea harusi ya mtoto wa chini ya miaka 18, ambaye licha ya kutakiwa kisheria awe darasani, wazazi wake walichagua kumwingiza kwenye ndoa, kwa malipo ya ng'ombe 10 na vijisenti kiasi cha 200,000.

Binti huyo mwanafunzi wa darasa la tano akiwa na miaka 15, alipatiwa mchumba mtoto mwezake mwenye miaka 17, ambaye angekabidhiwa mkewe baada ya kulipa mahari ya ng'ombe 10 na Shilingi 200,000.

Akizungumza na Nipashe, anasema kabla ya kuozwa alikatishiwa masomo, alikuwa darasa la tano katika Shule ya Msingi Manyada lakini wazazi wake wakahama kwenda Nzega mkoani Tabora akaendelea na masomo lakini safari hii katika Shule ya Msingi Ishiki iliyopo Nzega.

"Nikiwa sijamaliza darasa la tano mwaka 2020 wazazi wangu wakahamia tena kwenda mkoani Kigoma. Huko sikuendelea tena na masomo niliachishwa. Sikufahamu sababu pengine lengo lilikuwa ni kuletewa mwanaume nyumbani ili niwe mama na kuanza maisha ya ndoa, lakini si kusoma,"anaeleza binti.

Anasema wazazi wake walidai kuelemewa na maisha mwaka jana 2021, wakarudi tena kuishi kwa babu kijijini Manyada na tangu alipoachishwa masomo huko Nzega hakuendelea tena na masomo.

"Baada ya kukaa nyumbani ndipo wazazi wangu mwaka huu 2022 wakaniletea mchumba ili niolewe, huku tayari wakiwa wameshapokea mahari nami nilikubaliana nao kuolewa," anaongeza mtoto huyo.

### NDOA YATIBULIWA

Hata hivyo, ndoa yake ilitibuliwa na polisi na Maofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na anaeleza kuwa endapo atapata nafasi ya kusoma yupo tayari kuendelea na masomo ili atimize ndoto zake za kuwa mwalimu.

Anasema aliridhia kuolewa na mwanaume huyo ambaye hamfahamu vizuri wala haifahamu kazi yake ila alikutanishwa naye siku moja, lakini akishawishiwa na mama yake akubali kuolewa ili wapate mali na ikizingatiwa kuwa hasomi ndipo akakubali kwenda kuingia kwenye ndoa.

Mama yake (jina limehifadhiwa), anasema baada ya kuona binti yake yupo nyumbani muda mrefu na hasomi tena, ndipo wakaona ni bora kumwozesha mapema ili asije kupata mimba na kuwakosesha mifugo.

Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 inamtambua mtoto ni yule mwenye umri chini ya miaka 18, kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa mtoto, kwa kumpatia haki zake zote za msingi ikiwamo matunzo, chakula, malazi, mavazi, matibabu, pamoja na elimu bila ya kubagua jinsi yake.

Sheria hiyo ya mtoto baadhi ya wazazi mkoani Shinyanga wameipa kisogo na kutoitambua wakiendekeza tabia ya kukatisha masomo ya mabinti zao na kuwaozesha ndoa za utotoni ili wapate mifugo.

### BIHARUSI FEKI

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Shinyanga, Deus Mhoja, anasema tatizo ambalo limekuwa kikwazo kumaliza tatizo la ndoa na mimba za utotoni wilayani humo na Shinyanga nzima, ni jamii kuendekeza mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Anasema serikali inapambana kumaliza tatizo hilo lakini jamii bado imekuwa wagumu kubadilika na hata kufikia hatua ya kubuni mbinu mpya ya kufungisha ndoa za utotoni, kwa kuweka mabibi harusi feki ambao ni watu wazima ili wasikamatwe, lakini kumbe wahusika wamefichwa ndani na mabinti wanaozwa.

"Katika Halmashauri ya Shinyanga kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti mwaka huu tumeshatibua ndoa mbili za wanafunzi wakiwa ndani ya shela. Ya kwanza tuliitubua binti wa kidato cha tatu

INAENDELEA UK. 14

SAYANSI

NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA

# Una maoni kuhusu ubunifu, teknolojia?

## Yafikishe serikalini kwa kufanya haya...



Mmoja wa panya wanaogundua vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) akielekezwa kunusa sampuli zenye maradhi hayo. Ni moja ya kazi za ugunduzi na utafiti zinazofanywa nchini.**PICHA: MTANDAO**

DUNIA ya leo imepiga hatua kubwa katika nyanja ya sayansi na teknolojia inayofanikisha mapinduzi na maendeleo kiuchumi, kilimo, tiba na kwenye sekta zinazohusu maisha ya binadamu.

Huwezi kukwepa mabadiliko ndiyo maana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inafanya mapitio ya sera ya sayansi na teknolojia ya mwaka 1996, kuakisi mahitaji na kasi ya mabadiliko ya sasa yanayohusiana na dunia ya kielektroniki.

Akifungua mjadala wa kujadili na kupokea maoni ya wadau kuhusu rasimu ya sera ya sayansi, teknolojia na ubunifu na kiunzi cha uratibu wa masuala ya ubunifu nchini, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo, anatoa rai kwa wadau wa sekta hiyo kushiriki kutoa maoni ili kuchochea maendeleo ya taifa kupitia mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu.

"Kila Mtanzania mwenye maoni ambayo anadhani yanaweza kusaidia kuwa na sera nzuri ya taifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ayatoe ili kusaidia kasi ya maendeleo nchi na pia kuleta mabadiliko tunayoyatamani," anasema Prof. Caroline.

"Serikali imewekeza fedha nyingi kwenye Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STU), hii inatokana na umuhimu wake katika shughuli za kiuchumi na kijamii, nitoe rai kwa Watanzania kuendelea kutumia fursa zilizotolewa kutoa maoni ili kuhakikisha tunapata sera na kiunzi madhubuti kitakachojibu mahitaji na matarajio ya taifa letu," anasema Prof. Caroline.

Aidha, Prof. Caroline anaeleza mafanikio kadhaa yatokanayo na utekelezaji wa sera ya sayansi na teknolojia ya mwaka 1996, kuwa ni kuongezeka kwa taasisi za utafiti na maendeleo kutoka 18 mwaka 1961 hadi 94 mwaka 2021 na kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE).

Vilevile, imesaidia kuzalisha teknolojia mbalimbali zenye manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi, chanjo mpya za magonjwa ya mifugo, teknolojia rahisi ya kusafisha maji ya kunywa na uzalishaji wa mbegu mpya za mazao na wanyama.

Mafanikio mengine ni kupandishwa hadhi kwa Vyuo vya Ufundi vya Dar es Salaam kuwa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (MIST) kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na kuongezeka kwa idadi ya watafiti kutoka Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti na Maendeleo ya Umma kutoka 3,593 mwaka 2007/2008 hadi 10,966 mwaka jana.

Ushirikishwaji wa wadau ni jambo la msingi sana ili kufikia mafanikio ya kuwa na sera, kanuni na sheria nzuri zitakazochochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa maendeleo endelevu ya taifa.

> "Kila Mtanzania mwenye maoni ambayo anadhani yanaweza kusaidia kuwa na sera nzuri ya taifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ayatoe ili kusaidia kasi ya maendeleo nchi na pia kuleta mabadiliko tunayoyatamani," anasema Prof. Caroline.

Utekelezaji wa sera ya sayansi na teknolojia ya mwaka 1996 umechangia mafanikio mengi, lakini kutoka na mazingira ya sasa, kunapaswa kuwa na sheria iliyoboreshwa zaidi ili mipango ya serikali iweze kufanikiwa kikamilifu.

Mahitaji ya wataalamu waliobobea katika sayansi, teknolojia na ubunifu yameongezeka, hivyo ni lazima kuwa na sera nzuri itakayowezesha kufikiwa kwa mahitaji hayo. Wadau wa sayansi, teknolojia na ubunifu wanapaswa kushiriki kikamilifu kutoa maoni yao ili kupata sera nzuri itakayokidhi mahitaji ya nchi kwa wakati tulionao.

Viongozi serikalini, mashirika yasiyo ya kiserikali, asasi za kiraia, wanazuoni, viongozi wa dini, wanafunzi kuanzia shule za sekondari hadi elimu ya juu na wananchi kwa ujumla washiriki katika kutoa maoni yao.

Wapo wabunifu wengi nchini, ambao wanahitaji kuwekewa mazingira bora yatakayosaidia uendelezwaji wa ubunifu wao kwa maendeleo ya nchi, wanakaribishwa, anaongeza.

Wabunifu wengi hasa waliopo maeneo ya vijijini wanakabiliwa na tatizo la rasilimali fedha za kughramia ubunifu wao, hivyo wadau wanao wajibu wa kushauri uwepo wa sera ambayo itaujengea uwezo wa kifedha Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia ili kufadhili ubunifu kwani moja ya jukumu kubwa la mfuko huo ni kufadhili miradi ya utafiti na ubunifu nchini.

Ni ukweli kuwa, kama nchi Watanzania wanao wajibu wa kuendeleza kazi nzuri zinazoibuliwa na wabunifu wazawa ili wao nao washiriki kikamilifu katika programu mbalimbali za maendeleo.

Uibuaji na uendelezwaji wa ubunifu unapaswa kusimamiwa na sera madhubuti la taifa ambayo inakwenda na wakati na inaleta mafanikio kwenye kuibua, kuinua na kufanikisha kazi za kisayansi na teknolojia miongoni mwa Watanzania.

Ni vyema sasa kwa wadau kutoa maoni yao ili kuwa na sera bora ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Andiko hilo jipya litakapopatikana, litekelezwe ipasavyo ili kufikia malengo ya taifa ya kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kikamilifu katika shughuli za kila siku ili kurahisha kazi na muda kwa maendeleo endelevu katika kila nyanja.

***Mwandishi ni mwalimu wa Sekondari ya Mlali Sekondari iliyoko Kongwa, Dodoma.***
***Maoni: 0620-800462.***

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Wahadzabe 'wafalme wa msituni' waliobobea kulinda kila kiumbe

## Kuanzia mimea, maji hadi nyuki hawaumizwi

WENGI wanaosikia habari za Wahadzabe huenda wanawafikiria kwa mitazamo mbalimbali, wapo wanaodhani ni 'watu wa kale', ni viumbe 'wanaotisha' na baadhi wanadhani ni watu pori wasiofanana na Watanzania wengine.

Dk. Felician Kilahama, Mkurugenzi mstaafu wa Idara ya Misitu na Nyuki katika Wizara ya Maliasili na Utalii, ana majibu, alifika kwenye makazi ya Wahadzabe na leo anaanza simulizi, akigusia kwanza safari ilivyokuwa kwenda kwenye vijiji vyao.

Mwishoni mwa Februari na mapema Machi 2017, nilitembelea Wahadzabe katika sehemu wanapoishi Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, lengo kubwa lilikuwa kufanya tathmini ni kwa kiasi gani Wahadzabe wanatumia misitu kama maskani pia ikiwa ni sehemu muhimu ya kupata riziki za kila siku.



Dk. Felician Kilahama, akiwa na wenyeji wake Wahadza wakati wa ziara ya vijiji vya Domanga na Mong-wa-Mono. **PICHA ZOTE: DK KILAHAMA**

Haikuwa rahisi kufika eneo ambalo Wahadzabe wanaishi. Kwanza, kutoka Dar-es-Salaam mpaka Mbulu hadi Haydom ilichukua siku mbili.

Pili siku ya tatu nikateremka hadi kwenye 'Bonde la Ufa' katika eneo wanapoishi Wahadzabe. Safari ya Haydom hadi Yaedachini, ambako wanaishi, ilikuwa safari ngumu sana katika maisha yangu.

Sehemu kubwa ya barabara ilikuwa haionekani; tulimudu kufika kutokana na msaada wa Mwenyezi Mungu na uzoefu au ustadi wa dereva wa gari kwa kufanya maamuzi sahihi na kujua apite wapi.

Kuna mahali tulifika nikaambiwa ni mkoa wa Singida na baadaye kurejea tena eneo la Wilaya ya Mbulu.

Pamoja na hayo yote, ilikuwa safari ngumu sana; shukrani nyingi kwa Mungu Mwenyezi kwa kutuwezesha kufika huko na hatimaye kurejea Haydom salama.

Wahadzabe ni moja ya makabila 120 ya Tanzania, ambao wakati wa ukoloni walikuwa wakiishi katika eneo la Ziwa Eyasi katika mkoa wa Singida.

Hata hivyo, kufuatana na sera ya 'Ujamaa na Kujitegemea' na hatimaye kuanzisha Vijiji vya Ujamaa, hali hiyo ilipelekea baadhi ya Wahadzabe kuanzisha makazi yao katika sehemu za miinuko kwenye Bonde la Ufa wilayani Mbulu na maeneo ya Karatu.

Tathmini ya maisha ya Wahadzabe niliifanya mwaka 2017, katika eneo la Yaedachini, wilayani Mbulu.

Eneo hilo limegawanywa katika kata mbili za Eshkesh na Yaedachini zenye vijiji vitatu vya Wahadzabe lakini niliwasiliana nao katika vijiji vya Domanga na Mong-wa-Mono.

Hapo Yaedachini, sehemu ambayo ilikuwa na wakazi wachache wasio Wahadzabe; kwa hisani ya diwani wa eneo hilo nilipata sehemu ya kujihifadhi maana kulikuwa hakuna nyumba yoyote ya wageni.

### SIGARA TAMU

Namshukuru sana diwani (ingawa alikuwa akiishi Haydom) bila juhudi zake ingekuwa changamoto kubwa. Hakika, Mwenyezi Mungu alifanya njia pasipo na njia, jina lake lihimidiwe, nikiwa Haydom, nilishauriwa nisiende kwa Wahadzabe mikono mitupu ila niwe na paketi za sigara pia niwe na mtu anayefahamu lugha yao kuweza kutafsiri.

Nilijitahidi na kuzingatia ushauri huo na mambo yakaenda vizuri. Diwani alisaidia nikampata kijana mwenye pikipiki anayefahamu lugha yao pamoja na Kiswahili. Kutoka Yaedachini mahali nilipofikia hadi Wahadzabe walipo ni kama kilomita tatu. Hivyo, nilikuwa natoka asubuhi na kurejea jioni kwa kutumia pikipiki ya mkalimani.

Nikiwa huko msituni nilikutana na familia tatu, moja baba, mama na watoto wanne, kwa kila familia, baada ya kusalimiana na kutambulishwa, hawakuonekana wachangamfu, lakini baada ya kuwapatia paketi ya sigara hali ilibadilika na kila mmoja kufurahi mpaka watoto zaidi ya miaka mitano walichangamkia sigara.

Wahadzabe, wanaishi ndani ya msitu wa miombo iliyosheni zaidi miti ya mchanganyiko katika ikolojia ya "Acacia-Commiphora". Kimsingi ni wawindaji na wakusanyaji wa vyakula kutoka msituni, hawalimi wala hawafugi wanategemea mazao ya msituni kwa maisha yao ya kila siku.

Katika mazungumzo yangu nao na baada ya kutembezwa sehemu kadhaa msituni ilidhihirika kuwa Wahadzabe ni watunzaji wazuri wa msitu wanaoutegemea kwa maisha yao ya kila siku. Kwa kufuatana na majira mbalimbali, wanaweza kuishi wakipata chakula na lishe ili kutosheleza mahitaji yao.

Hata hivyo, walieleza kuwa kwa miongo miwili iliyopita hali ya upatikanaji wa chakula cha kutosha imekuwa changamoto kubwa kwao. Moja ya visababishi ni kuongezeka kwa ujangili na vilevile, kasi ya mabadiliko ya tabianchi imesabaisha hali ya ukame kuongezeka na kuathiri upatikanaji wa chakula na pia wanyama kupungua.

Maongezi yangu na Wahadzabe yalionyesha kwamba kutoka msituni wana asali, mboga asilia, matunda kwa majira tofauti, wanachimba mizizi ambayo waliita mihogo au viazi vya asili lakini pia wanao utamaduni wao na mgawanyo nzuri wa kazi na kuwajibika. Wanaume wakijikita zaidi katika kuwinda wanyama na kurina asali; wakati wanawake wakishughulikia maji, kutafuta mboga na kuchimba "mihogo au viazi" sehemu mazao hayo yanapopatikana.



Wavulana wadogo kati ya miaka mitano hadi 10 pia wanaweza kuwinda wanyama wadogo na ndege pia, kukusanya matunda hasa kutoka kwenye miti mikubwa kama mibuyu (Adansonia digitata). Wanawake kadhalika wanarina asali hata kutoka kwenye miti ambayo siyo mikubwa.

Uwindaji wa wanyama unafanyika kwa kutumia upinde na mishale (baadhi yake huwekwa sumu) kusaidia kuwauwa wanyama wakubwa kwa urahisi. Watoto wanatumia manati kuua ndege na wakati mwingine kuwatega kwa kutumia nyaya kwa mbinu zao za asili.

### URAFIKI NA MAZINGIRA

Kusema kweli Wahadzabe wamekuwa wakiishi vizuri na mazingira yanayowazunguka. Hawafyeki msitu au kukata miti hovyo Wakati tunatembea msituni niliona nyoka nikashtuka, aliyekuwa ananiongoza akanipa moyo akisema usihofu hakuna shida, ikitokea bahati mbaya akakugonga, dawa za kuondoa sumu zipo msituni, utakuwa salama (dhana ya binadamu na mazingira).

Vilevile, wanapojenga nyumba zao hawakati miti wanatumia matawi na nyasi na ujenzi wao ni kwa matumizi ya muda tu hasa nyakati za mvua.

Kwa majira mengine wanaweza kulala tu chini ya mti bila adha yoyote (bila kuogopa wanyama au nyoka). Baada ya maelezo mazuri nikapata picha kamili jinsi wanavyotumia rasilimali misitu kumudu maisha yao ya kila siku bila kuathiri uhai wa mazingira ya msituni.

Kwa hali hiyo wamejenga uelewa mzuri na ujuzi wa asili kuhusu mazingira ya msitu wanapoishi

Nyumba zao ni za muda tu maana wanasema hawaishi sehemu moja kwa muda mrefu, wanahamahama kulingana na upatikanaji wa chakula. Wahadzabe hawana tabia ya kuchoma moto msitu kwa sababu ndiyo ghala la chakula.

Kwa uzoefu wao wa miaka mingi wanaweza kutengeneza zana zao kama mishale na upinde kuwindia wanyama kwa kuzingatia utamaduni wao wa kuwinda na kukusanya vyakula mbalimbali na asali.

Kuhusu asali wahatengenezi mizinga isipokuwa wanajua sehemu asilia ambazo nyuki huzitumia kutengeneza asali kwa nyuki wanaouma na wasiouma. Katika Makala itakayofuata nitafafanua zaidi jinsi Wahadzabe wanavyotumia mazingira ya msituni, kuishi na kuyamudu maisha yao kila siku bila kuathiri ikolojia yake kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

*ITAENDELEA JUMMANE IJAYO*

# Aliyetibuliwa mpango wa kuozwa asimulia mwanzo, mwisho mambo yalivyokuwa

INATOKA UK. 11

ambaye alikuwa akisoma katika Shule ya Sekondari Itwangi, na hii ya sasa ya Kijiji cha Manyada wote utaratibu umefanyika ili waendelee na masomo yao," anaongeza Mhoja.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Aisha Omary, anasema uvamizi wa ndoa za utotoni na kuwakamata watuhumiwa, umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matukio ya ndoa za utotoni wilayani humo, ambako kipindi cha nyuma ndani ya mwaka mmoja wanafunzi 20 walikuwa wakiozeshwa, lakini idadi imepungua ni takriabni wanne.

Mkurugenzi wa Shirika la Agape, John Myola, ambaye anapambana kutokomeza ndoa za utotoni mkoani Shinyanga, analaani wazazi mkoani humo kuendelea kuwadharau watoto wa kike na kumgeuza kitega uchumi cha familia kwa kumuoza ili wapate mifugo na fedha.

Anasema watoto wa kike wana akili kimasomo, lakini anashangaa baadhi ya wazazi mkoani Shinyanga kuwadharau na kuamua kuwakatisha masomo na kuwaozesha ndoa za utotoni na kuharibu mustakabali wa maisha yao.

"Kwenye shirika letu tunaishi na watoto ambao wamepata mimba na kuingizwa kwenye ndoa za utotoni, na nina wasomesha kwa mfumo rasmi na wengine usiyo rasmi na wana uweo , baadhi yao wapo vyuoni kwa sasa na wengine kidato cha tano na sita, lakini walikuwa kwenye ndoa tukawaokoa,"anasema Myola.

"Nawasihi wazazi na walezi waache tabia hii ya kuozesha watoto ndoa za utotoni, licha ya kutaka mali wafikirie kwanza utu wa mtoto. Mwanao bado ni mdogo unampeleka kwenye majukumu ya ndoa na wakati watu wazima waliomo kwenye ndoa wanazikimbia," anaongeza Myola.

Sonda Kabeshi ni mzee wa kimila, anasema tamaduni hizo ni za kizamani sana, siku hizi watoto wa kike wanasomeshwa na wanasaidia kikamilifu familia zao kuliko hata wakiume na ameshuhudia wengi akiwashauri wazazi waachane na mila za kizamani, wasiozeshe watoto ndoa za utotoni bali wawache wasome na kutimiza ndoto zao.



Wazazi na walezi wa mkoa wa Shinyanga wawasaidie wasichana kusoma ili kumudu maisha yao badala ya kuwalazimisha kuolewa kwa nia ya kupata mifugo na pesa. **PICHA: MAKTABA**

Mratibu wa Mpango Mkakati wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto mkoani Shinyanga, Tedson Ngwale, anabainisha mikakati ya serikali katika kukabiliana na tatizo hilo la ndoa za utotoni, kuwa ni pamoja na kutunga sheria ndogo ili kudhibiti ufungishaji wa ndoa hizo.

Anasema vipengele vya sheria hiyo ndogo vitakuwa ni kujaza fomu pamoja na kufanya tathmini ya ndoa kabla ya kufungwa, ili kujiridhisha kama ndoa hiyo haozeshwi mtoto pamoja na kuangalia miaka yake katika vyeti vya kuzaliwa, hali ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kutokomeza ndoa za utotoni mkoani Shinyanga.

"Fomu za ndoa zitakuwa zikipatikana kwenye ofisi za watendaji wa vijiji na sheria hii ndiyo itakuwa mwarobaini wa kutokomeza ndoa za utotoni hapa Shinyanga na kuufanya mkoa huu kuwa wa mfano kwenye kuheshimu haki za watoto," anasema Ngwale.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, katika ukurasa wake wa Instagram, analaani kuendelea kwa matukio ya ndoa za utotoni mkoani Shinyanga na kupongeza jitihadi ambazo zimekuwa zikichukuliwa dhidi ya kukomesha ndoa hizo ikiwamo uvamizi wa sherehe na kuzitibua.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) mwaka 2012, Shinyanga inaongoza kwa ndoa za utotoni asilimia 59, ikifuatiwa na Tabora 58 na mkoa wa Mara ni watatu kwa asilimia 55.

## WANENAVYO MALENGA

### KWANINI ZAFUNGWA SHULE?

HILI waliangalie, kwanini zafungwa shule,
Majibu tupatie, kwanini zingine shule,
Kufungwa wasisikie, watoto waende shule?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Na sasa tuangalie, amri zifungwe shule
Watoto wasubirie, hesabu ya sensa ile,
Kwa vipi tuwaambie, wengine waende shule?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Wahusika tuambie, kweli mnafunga shule?
Semeni msitanie, mbona wengi wenda shule?
Wapi wapumzikie, kama siku zote shule?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Vipi msifikirie, shule za zamani zile,
Elimu muisifie, ilokuwa juu ile?
Wenyewe tufurahie, likizo likizo zile?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Ni kwa nini tusifie, kuhusu elimu ile,
Ya sasa tuisagie, kwamba siyo kama ile?
Pengine tufikirie, nje ya boksi lile,
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Wivu sinifikirie, kwa wanaosoma wale,
Lakini ufikirie, wapi pumziko lile,
Watoto wajisikie, kitabu kibaki shule?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Wengine nisaidie, na hizi zangu kelele,
Ama mnifagilie, au yangu tupa kule,
Lakini mniambie, tunaenda nyuma mbele?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

Watoto tuangalie, kwa uraibu wa shule,
Maisha tuangalie, yapo zaidi ya shule,
Tukwepe wasisalie, yote wafanye kishule,
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

La nne waangalie, mwaka mzima ni shule,
Ni nini tujipatie, wasipumzike wale?
Ndivyo tuwasaidie, au wabakie lele?
Kwanini shule zifunge, zingine ziendelee?

La saba niwatajie, mashindano ya kishule?
Ticha nini umwambie, adhabu kufeli kule?
Mzigo tuwamwagie, watoto kubaki shule?
Kwanini shule zifunge, zingine waendelee?

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# Sababu kukwama elimu jumuishi zatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

PAMOJA na serikali kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji elimu bora, bado kuna kero zinazokwamisha programu za elimu jumuishi kwa watoto wenye ulemavu, imeelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Child Support Tanzania, Noela Msuya, alibainisha hayo juzi jijini hapo kwenye mkutano wa kitaifa wa majadiliano kuhusu elimu jumuishi.

Alisema kero zinazowakabili watoto wenye ulemavu kupata elimu ni pamoja na kukosekana kwa mfumo wa kupima vipaji kwa watoto, uhaba wa walimu na wataalamu wa elimu jumuishi na vifaa saidizi.

Aidha, alisema lengo lao ni kukuza uelewa na kuhakikisha wanapata elimu bora katika mfumo wa elimu jumuishi.

"Child Support Tanzania tunaamini katika mambo manne usawa kwa watu wote lakini tunaamini ulemavu si kushindwa. Tunaamini katika utendaji wa kijamii. Kazi zetu zote tunaamini inapohusishwa zinaweza kwenda vizuri zaidi na kuwa na mwendelezo pamoja na kuthamini vipawa, vipaji kwa watoto wenye ulemavu," alisema.

Msuya aliongeza kuwa tangu wameanza kazi zao miaka 14 iliyopia, wamewafikia zaidi ya watoto 1,000 wenye mahitaji maalumu ambao wamewapeleka shuleni.

Awali, akifungua mkutano huo, Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, alisema elimu jumuishi itasaidia kuwawezesha watoto wenye ulemavu kupata elimu itakayowasaidia kupiga hatua ya kuondokana na ujinga na umaskini huku akibainisha juhudi zilizofanya na serikali hadi sasa.

Dk. Tulia alisema watashirikiana na shirika hilo pamoja na serikali kuhakikisha elimu jumuishi inapewa kipaumbele.

"Nitoe wito kwa taasisi na mashirika mbalimbali kujifunza kutoka kwa Shirika la Child Support Tanzania. Nafurahi kuona wako tayari kutoa uzoefu wao katika kuhakikisha jamii zetu zinakuwa bora zaidi kuliko ilivyosasa kwa maana ya kutoa elimu hii jumuishi," alisema Dk. Tulia.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mkutano huo, Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi na Wasioona, David Shaba, aliitaka serikali kuwajali wenye ulemavu kwa kuwapa elimu sambamba na kutenga bajeti ya kufadhili wenye ulemavu kwa fedha za ndani badala ya kutegemea wafadhili kutoka nje.

"Naomba ulivalie njuga suala hili la watu wenye ulemavu kupata elimu. Kuna umuhimu mkubwa wa kutengewa bajeti kwa sababu miradi mingi inakwama kwa kukosa ufadhili na hatuwezi kutegemea wafadhili kutoka nje ya nchi wakati rasilimali zote tunazo," alisema.

Vilevile, mwenyekiti huyo aliomba kwa niaba ya watu wenye ulemavu kutengewa bajeti maalumu.

## Bunge lapongeza utendaji kazi TBA

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Miundombinu, imepokea, kujadili na kushauri taarifa ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhusu masuala mbalimbali ya kiutendaji ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na kuupongeza kwa utendaji wake katika miradi mbalimbali.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa ya utendaji kazi wa TBA, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Moshi Kakoso, alitoa pongezi na kuridhishwa na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na wakala huo.

Kakosi alisema kamati imeridhishwa na utekelezaji wa miradi yao, ila wahakikishe wanaweka mikakati inayotekelezeka kwa kuwa uwekezaji kwenye ujenzi wa nyumba unakuwa wa kubadilika kila siku.

"Mnatakiwa mwende sambamba na mabadiliko hayo ili kupata wateja ndani na nje ya nchi. Ninaamini mtaweza kutokana na uchapakazi wenu," alisema Kakoso.

Aidha, Kakoso aliitaka TBA kuhakikisha inaendelea kubuni miradi mbalimbali katika maeneo ambayo wanamiliki ili kulinda maeneo yao pamoja na kusambaza huduma kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Alisema wakifanya hivyo itawasaidia kuendelea kupata wateja wengi kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisisitiza TBA kuendelea kuwa wabunifu kwa kuhakikisha inaendelea kujenga na kukarabati nyumba na majengo ya serikali ili kuongeza ubora wa makazi kwa viongozi na watumishi wa umma.

Waziri Mbarawa aliitaja miradi mikubwa ya kitaifa ambayo imetekelezwa na TBA kuwa ni ujenzi wa nyumba za makazi za Magomeni Kota, jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sekou Toure Mwanza, jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, ujenzi wa makazi ya Rais mstaafu wa Awamu ya Nne na usimamizi wa mradi wa ujenzi wa Ikulu, Chamwino Dodoma.

Alisema wizara hiyo itaendelea kuwa mstari wa mbele ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii kiendeleza miradi ya maendeleo hapa nchini.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua jengo la Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu, wakati alipokagua maendeleo ya ujenzi wa majengo ya wizara mbalimbali katika Mji wa Serikali-Mtumba, Dodoma juzi. P**ICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mradi miji 28 kumaliza tatizo la maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema mradi wa maji wa miji 28 wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 unaotekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini, utasaidia kutatua tatizo la maji mijini na vijijini na kupunguza magonjwa ya mlipuko.

Aidha, miji itakayonufaika ni pamoja na Handeni, Muheza, Pangani, Kilwa Masoko, Newala, Ifakara, Chunya, Songea, Njombe, Rujewa.

Miji mingine ni Makambako, Wanging'ombe, Mafinga, Nanyumbu, Mpanda, Sikonge, Urambo, Kaliua, Singida, Manyoni, Chemba, Chamwino, Kasulu, Kayanga, Geita, Rorya, Tarime na Chato.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Maji, Juma Aweso, iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Habari, Frolence Temba, Watanzania takribani milioni sita watanufaika kwa kuimarishiwa huduma ya majisafi na salama.

Alisema sekta ya maji imekuwa ikitoa utatuzi katika maisha ya kila siku ya wananchi.

"Mradi wa maji wa miji 28 ni moja ya miradi mikubwa inayotekelezwa na serikali na kazi inafanikishwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka serikali ya India, kupitia Benki ya Exim ya India ukiwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 500 sawa na zaidi ya Sh. trilioni moja. Hii inaonyesha wazi dhamira ya serikali kumtua mama ndoo kichwani imetimia," alisema.

Hata hivyo, kazi ya utekelezaji wa mradi huo imetolewa kwa kampuni tofauti, hali ambayo inamaanisha kuwa itakamilika mapema zaidi na wananchi kunufaika na jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita.

"Lengo la serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa maji kwa maeneo ya vijijini ifikie asilimia 85 na mijini asilimia 95. Mweleko ni mzuri, tunafanya kazi saa 24 ili wananchi wapate suluhu. Hatutaki kuwa kikwazo katika jambo hili muhimu," alisema.





# Wahitimu Chuo cha Ujenzi waitwa fedha za miradi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

VIJANA waliohitimu katika Chuo cha Ujenzi wa Miundombinu ya barabara kwa kutumia teknolojia stahiki ya nguvu kazi cha Institute of Construction Technology (ICOT), wametakiwa kujiunga kwenye vikundi ili waweze kupatiwa fedha kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara za vijijini.

Wito huo ulitolewa juzi na Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini Wilaya ya Rungwe, Mhandisi Abidinico Massaba, wakati akifunga mafunzo ya ujenzi wa barabara kwa wanafunzi 13 kutoka mikoa mbalimbali nchini waliohitimu mafunzo kwenye chuo hicho.

Alisema chuo hicho kina jukumu la kuwafundisha vijana ujuzi wa kutengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe, upimaji wa barabara na makaravati na kufanya ukaguzi wa mradi kabla ya kuanza shughuli za ujenzi.

Alisema chuo hicho ni msaada kwa wananchi kupata maarifa ambayo yamewasaidia kujiajiri au kuajiriwa na kampuni mbalimbali ya ujenzi.

"Serikali haiwezi kukidhi mahitaji ya ajira nchini, kutokana na hali hiyo chuo chetu kikaanzisha mafunzo haya ya muda mfupi kwa ajili ya kuwapa ujuzi wananchi juu ya utengenezaji wa barabara, makaravati na shughuli nyingine ambazo mtu akifanikiwa kujifunza vizuri anaweza kujiajiri na kuingiza kipato," alisema Mhandisi Massaba.

Mkuu wa Chuo hicho cha Institute of Construction Technology Mbeya (ICOT), Mahamud Chamle, alisema teknolojia stahiki ya nguvu kazi ni msaada mkubwa kwa Watanzania waliopatiwa mafunzo hayo kutokana na kurekebisha barabara ambazo ni muhimu kuwasaidia wakulima.

Alisema wanafunzi hao wanatakiwa kutumiwa na wakala wa barabara za mijini na vijijini (TARURA) kwa kuwa wameshapatiwa ujuzi huo wa kutengeneza barabara ambazo zitasaidia kusafirisha mazao kutoka vijijini hadi yalipo masoko.

Alisema chuo hicho kinatoa nafasi kwa wananchi kujifunza ujuzi wa utengenezaji wa barabara kwa kutumia teknolojia ya kawaida na kuisaidia jamii katika maeneo wanayoishi.

Mmoja wa wahitimu wa mafunzo hayo, Jackline Alphonce, alisema pia wamefundishwa namna ya kuandaa mpango kazi ambao utawasaidia kuomba miradi na zabuni.

"Licha ya kupatiwa mafunzo hayo ambayo yametuwesha kupata ujuzi utaotusaidia kuendesha maisha yetu huko mtaani, lakini chuo chetu kina mahitaji mbalimbali kwa ajili ya kuendesha shughuli zake kama vile magari kwa ajili ya kutuwezesha wanafunzi kwenda kufanya mafunzo ya vitendo pamoja na vifaa vya usalama mahali pa kazi," alisema Alphonce.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, Dk. Vicent Anney, akitoa salamu za serikali kwa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Busokelo wilayani humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Waomba ujenzi miundombinu uzingatie wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa elimu jijini hapa wamewaomba wataalamu wanaotekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kuzingatia miundombinu ya watoto wenye ulemavu ili waweze kusoma kwa raha na kutimiza ndoto zao.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mdau wa elimu mkoani hapo, Thabitha Bugali, alipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya miundombinu ya elimu kwa watoto wenye ulemavu.

"Tulijaribu kutembelea baadhi ya shule za msingi vijijini tukabaini miundombinu ya shule husasani vyoo havisapoti watoto wenye ulemavu kupata huduma, tunaishukuru serikali kwa mwongozo mpya walioutoa kuhusu namna bora ya kujenga ikizingatia miundombinu ya watu wenye ulemavu," alisema Bughali.

Alisema kuna kila sababu serikali inapopata wahisani wa kuwekeza katika sekta ya elimu na kwamba wajikite zaidi maeneo ya vijijini ili kuboresha miundombinu ya vyoo vikidhi mahitaji kwa kuzingatia watoto wenye ulemavu.

Mkazi wa Mama John, Jaqline Sanga, alisema kuwa licha ya kuwapo kwa vikwazo mbalimbali vinavyowakabili watoto wenye ulemavu shuleni, lakini jamii inapaswa kushirikiana na serikali kwa kutumia nguvu kazi katika kuboresha miundombinu ya vyoo, vyumba vya madarasa badala ya kuiachia jukumu hilo serikali pekee.

Mwenyekiti wa Chama cha Wenye Ulemavu Mkoa wa Mbeya (CHAWATA), Jimmy Ambikile, alisema bado kuna tatizo kwenye suala la miundombinu kwa wenye ulemavu kuanzia shule za msingi hadi sekondari.

Vilevile, alisema hata kwenye majengo ya taasisi mbalimbali za umma hakuna miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu na suala hilo lifanyiwe kazi ili nao wapate huduma bila vikwazo.

# W'biashara wa miwa wafurahia mazingira soko jipya

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa miwa katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, waliohamishwa kutoka soko la Soweto kwenda uwanja wa ndege wa zamani, wameeleza kufurahishwa na mazingira mapya ya biashara kwa kupata eneo kubwa linalowawezesha kuhudumia wateja wengi.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Manijala Kibona, akiongea na Nipashe kuhusu mazingira mapya ya biashara, alisema baada ya uongozi wa jiji kuwahamishia mahali hapo wanaona wamepata eneo sahihi kwa ajili ya biashara hiyo.

Kibona alisema soko la miwa la uwanja wa ndege wa zamani ni zuri na la uhakika ikilinganishwa na Soweto ambalo eneo la kufanyia biashara lilikuwa halikidhi mahitaji yao na wateja wao.

Alisema kutokana na mazingira mazuri waliyoyapata, kwa sasa biashara yao ya miwa imekuwa nzuri, kiasi cha kuwawezesha kupata idadi kubwa ya wateja na kuongeza kipato chao.

"Biashara ya miwa kwa sasa imekuwa nzuri sana, kwa kuwa bidhaa zetu tunazipanga vizuri, eneo ni kubwa na kutokana na uwepo wa stendi ya mabasi jirani, hata idadi ya wateja wetu imeongezeka," alisema Kibona.

Alisema kwa sasa ana uwezo wa kukusanya faida ya Sh. 10,000 kwa siku moja ikilinganishwa na ilivyokuwa Soweto faida ilikuwa ni Sh. 5,000 kwa siku.

Anna Masebo alisema baada ya Halmashauri ya Jiji kutenga eneo alihamishia biashara yake kutoka kuwa machinga aliyekuwa anatembeza mtaani.

Alisema kwa sasa ana uhakika wa biashara yake kwa kuwa wateja wapo wa kutosha na anapata fedha za kujikimu kimaisha na kumuwezesha kusomesha watoto.

Alisema kikwazo kilichopo kwa sasa kwenye biashara yake ni gharama kubwa ya kununua mzigo shambani ikilinganishwa na faida wanayoipata.

Hivi karibuni Mbunge wa Jimbo la Mbeya ambaye ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, aliwaahidi wafanyabiashara waliohamishia biashara zao eneo la uwanja wa ndege ilipo stendi ya mabasi kujengewa miundombinu rafiki ikiwamo barabara na vyoo vya kisasa.

Aliwasisitiza wafanyabiashara kuendelea kulipa ushuru, kutunza mazingira ili serikali itimize wajibu wake wa kuwahudumia wananchi kwa kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akiwa mkoani Mbeya, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Watoto na kundi maalum, Dk. Doroth Gwajima, aliwataka wafanyabiashara kujiunga kwenye vikundi ili kupata mikopo ya asilimia 10 kutoka halmashauri.

Alisema halmashauri ina fedha, lakini kinachozingatiwa kukopesha vikundi vitakavyokidhi vigezo ikiwamo kuwa na biashara inayoeleweka, kusajiliwa, kutambulika na ofisi za mitaa pamoja na malengo yaliyokusudiwa.



# Ufaransa kuboresha Uwanja wa Ndege Amani Karume

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imetiliana saini ya hati ya makubaliano ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa jengo jipya la abiria 'Terminal 4' katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, mjini hapo.

Hafla ya utiaji saini hati ya makubaliano hayo imefanyika katika ofisi za wizara hiyo Kisauni kati ya Katibu Mkuu, Khadija Khamis Rajabu, ambaye ameiwakilisha wizara na Eric Fluerisson, Mkurugenzi Mtendaji aliyeiwakilisha Kampuni ya Bouygues kutoka nchini Ufaransa.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema serikali imeamua kujenga jengo jipya la abiria ili kutatua changamoto iliyoko ya kuzidiwa jengo la abiria namba tatu wakati wa kushusha abiria katika kiwanja hicho.

Waziri Dk. Khalid alisema upembuzi yakinifu utakaofanyika hautoigharimu serikali kiasi chochote cha fedha na badala yake serikali italazimika kutoa wataalamu wake ili kushirikiana na kampuni hiyo.

Alisema, dhamira ya serikali ni kujenga jengo litakalokidhi mahitaji kwa zaidi ya miaka 20.

Alisema wizara inakusudia kuyafanyia kazi maono ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kwa vitendo kwa lengo la kuifungua Zanzibar kupitia sekta ya miundombinu.

Alisema azma ya Dk. Mwinyi kuifungua Zanzibar kiuchumi kupitia sekta ya miundombinu katika kuimarisha miundombinu hiyo inajumuisha sekta ya anga kwa kuviendelea viwanja vyake vya ndege.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji kutoka Kampuni ya Bouygues, Eric Fleurisson, alisema wanaishukuru serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kuwapatia kazi hiyo na kitendo hicho kinadhihirisha imani kubwa waliyo nayo kwa kampuni yao.

Eric aliuhakikishia uongozi wa wizara kuwa wataifanya kazi hiyo kwa haraka na uhakika kwa kushirikiana na watendaji kutoka wizarani na wafanyakazi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar.



Waandishi wa habari visiwani Zanzibar wakimsikiliza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), wakati akizungumza nao jana, Ikulu visiwani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ripoti ya CAG kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka wa fedha 2020/2021 inatarajiwa kuwasilishwa katika mkutano wa nane wa Baraza la kumi la Wawakilishi, litakaloanza Septemba 7, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Mselem, alisema katika mkutano huo pia kutawasilishwa na kujadiliwa kwa miswaada miwili ya sheria.

Alitaja miswada hiyo kuwa ni wa kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (kinga, uwezo na fursa) namba 4 ya 2007 na kutunga sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Alisema sheria hiyo imepitwa na wakati na inahitaji marekebisho ili kuendana na wakati wa sasa.

Pia alisema mswaada wa sheria ya kuanzisha taasisi ya wahasibu, wakaguzi na washauri elekezi wa kodi Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Kadhalika, ripoti za wizara zote za serikali zitawasilishwa kuhusu utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati za kudumu za baraza kwa mwaka 2021/2022.

Kutakuwa na maswali na majibu 159 na taarifa ya serikali kuhusu mchezo wa ngumi Zanzibar.

**Alisema sheria hiyo imepitwa na wakati na inahitaji marekebisho ili kuendana na wakati wa sasa.**

# Kampuni yajitokeza kununua mwani kwa bei ya juu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Mwani Zanzibar (ZASCO), inatarajia kununua mwani wa Spinosam na Kotonii kwa bei kubwa kwa wakulima wa zao hilo ili kuwaongezea kipato.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Dk. Masoud Rashid Mohammed, alisema bei hiyo itakuwa kubwa ikilinganishwa na iliyopo sasa ili kutekeleza dhamira ya serikali ya kunyanyua wananchi wake kiuchumi kupitia sekta ya uchumi wa buluu.

Alisema Rais Dk. Mwinyi katika kampeni alitoa ahadi kwa wakulima hao kuwainua kiuchumi, kuwatafutia masoko na kuongeza bei ni moja ya ahadi zake.

Akizungumzia uzalishaji wa zao hilo, alisema kwa mwaka 2021 zaidi ya tani 10,000 zililimwa na uzalishaji ulikuwa mkubwa zaidi mwaka 2015/2016 kwa tani 15,000 kulimwa.

Aliwaomba wakulima kuendelea kulima zao hilo na kuwahakikishia kuwa kampuni hiyo itanunua mwani huo kwa bei iliyo bora zaidi baada ya kiwanda hicho kukamilika.

"Kwa vile sasa serikali imeanza ujenzi wa kiwanda cha mwani huko Chamanagwe, uwezo wake ni kuchakata mwani zaidi ya tani 30,000 kwa mwaka hivyo wajitahidi kulima mwingi zaidi ili kiwanda chao kisije kufeli na kiweze kupata wa kutosha," alisema.

Mwenyekiti wa wakulima wa zao hilo, Pavu Mcha Khamis, aliishauri kampuni hiyo itakaponunua kuhakikisha unakuwa safi na upo vizuri.

"Wanaweza kuchukua mwani baharini vizuri na kuutunza vizuri, lakini siku ambayo anakwenda kuuza akatia jiwe lenye zaidi ya kilo tano katikati ya mwani sasa hilo ni angalizo ambalo naishauri kampuni wakati wa kununua wawe makini ili wasije wakauziwa mchafu na vitu visivyohitajika," alishauri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE

Kituo cha..................Mkoa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa Mirathi Na. 1665 / 2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWISHEHE MGOLELE GABRIEL
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHABANI MWISHEHE MGOLELE

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 Mwezi wa 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 02 Mwezi wa 09 Mwaka 2022.**

HAKIMU

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR ES SALAAM

## KUPOTEA KWA CHETI



**COLLIN FRANK KIDOGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5201/0013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST JOSEPH BOYS SCIENCE SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/350756/2022**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**HAJI ABEID POSSY** anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S2858-0138** iliyotolewa na **SUA SEKONDARI** Novemba, 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: DAR/KIM/RB/350906/2022.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

OFIFI YA HAKIMU MKAZI MFAWIDHI

MAHAKAMA YA WILAYA MASASI
S.L.P 88
MASASI

KUITWA SHAURINI

MADAI YA RUFAA NO. 05/2022

MDAI: ISSA MOHAMED NGUYAHAMBI

MDAIWA: SAIDI SAIDI MATOGORO

Madai haya yamefunguliwa katika mahakama hii. Ndugu SAIDI SAIDI MATOGORO unaamriwa na mahakama hii kuhudhuria mahakamani mnamo tarehe 12/09/2022 na usipo hudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.
Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 09 mwaka 2022 hapa mahakama ya Wilaya Masasi.

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA
MASASI

## KUPOTEA KWA CHETI



**MEDRINA MORGAN MWAIJULU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **No. S4993-0081** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia RODAN SECONDARY SCHOOL mwaka 2019.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MWA/NYA/RB/239464/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALLY KOBE KUMBIKILA** inatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 572 CLM – BOXER.** Chassis namba **MD2A21BY2KWH97419.** Engine namba **PFZWKH55238.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/895/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANNA THOMAS NAGUNWA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 839 BKM TOYOTA SPACIO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/351955/2022**

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO

DISTRICT AT MOROGORO

PROBATE AND ADMINISTRATION

CAUSE NO 93 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late:
EPHRAIM NJAWALLA MWAMPAMBA

BY 1. ANISOARA A. MWAMPAMBA

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of SEPTEMBER.........2022

Dated at MOROGO this **5 day of SEPTEMBER.........2022**

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EPHRAIMU DAMIAN LIGATE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 912 CVU.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/352195/2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MOROGORO MJINI
KITUO CHA KIHONDA, MKOA WA MOROGORO
SHAURI LA MADAI Na....2022
JINA LA MDAI: LEMUNYO MLIGO
JINA LA MDAIWA: RASHID KALESHI

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)

**Kwa:RASHID KALESHI, HENJEI KIDAHABU, KIDUYA MATI,MUSSA MASUJA ATHUMANI................WADAIWA**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Madai ya pesa kiasi cha sh.11,200,000/=.Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 12/09/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:**Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 02/09/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NOAH MESHACK MOSHI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T837AMM** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0679142593** **DSM/PHQ/RB/349630/2022**

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 120 OF 2022

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ISAYA MALYOSI UPAMBA Madukani Ward within City Council of Dodoma

AND

IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION
BY RABEKA ISAYA UPAMBA

**GENERAL CITATION**
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admiration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **28th Day of SEPTEMBER, 2022.**

**Dated at Dodoma this 30th day of AUGUST, 20**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI


**YOHANA MSAPA SICHONE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki aina ya Boxer yenye namba za usajili **MC 501BCV** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0713181505 /0744642464** **MOR /MOR/RB/345029/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EZRON SOSPETER ALBINUS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0136/0043** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MUSOMA SECONDARY SCHOOL mwaka 2020 . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **MWS/RB/6678/22**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*




**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waziri mkuu Uingereza kujulikana wiki hii

**LONDON, UINGEREZA**

WAZIRI wa mambo ya nje wa Uingereza Liz Truss anatarajiwa kuwa waziri mkuu mpya wiki hii baada ya kura kupigwa na chama cha Konsavative.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, Truss aliahidi kuchukua hatua ndani ya wiki moja baada ya kuchaguliwa kushughulikia suala la kupanda kwa gharama za maisha kulikochochewa zaidi na kupanda kwa bei ya mafuta kufuatia mapigano ya Ukraine.

Akizungumza na shirika la habari la BBC Jumapili Truss, hakueleza kwa kina kuhusu hatua anazokusudia kuchukua.

Pia, Truss alisema kwamba anaelewa matatizo yanayoikumba Uingereza yakiwamo serikali kushindwa kushugulikia suala la kushuka kwa thamani ya sarafu yake, mazingira ya wafanyakazi pamoja na mfumo wa afya usio thabiti, tangu Julai baada ya waziri mkuu Boris Johnson kutangaza nia yake ya kujiuzuru, suala lililosababisha kampeni kali za kutafuta mrithi wake.

Chama cha Konsavative kinatarajiwa kutangaza mshindi atakayechukua nafasi ya Jonhson Jumatatu, ambapo Truss anapambana na Rishi Sunak, waziri wa zamani wa fedha kuwania nafasi ya waziri mkuu wakati atakayeibuka mshindi pia akifanyika kuwa mkuu wa chama hicho.

Aidha, ilielezwa kuwa wakati wa kampeni, Truss aliahidi kuongeza matumizi ya fedha za ulinzi, kupunguza kodi pamoja na kuongeza nishati, ingawa hakueleza kwa kina anavyokusudia kutekeleza hayo.

**VOA**

# Mahakama Kenya yaidhinisha ushindi

**NAIROBI, KENYA**

MAHAKAMA ya Juu imeidhinisha uchaguzi wa William Ruto, kuwa Rais mteule wa Kenya huku majaji wakiongozwa na Jaji Mkuu Martha Koome wakieleza kwamba, ushahidi uliotolewa na mlalamikaji Raila Odinga ulikuwa umejaa uvumi na porojo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, uamuzi wa majaji ulikuwa ni wa jumla ulioungwa mkono na wote, ndani ya siku 21 za kutolewa kwa uamuzi huo.

Jaji Martha, alisema mahakama hiyo ya nchini Kenya imetupilia mbali pingamizi la mwanasiasa Raila Odinga kupitia muungano wa kisiasa wa Azimio ambao ulikuwa unapinga ushindi wa William Ruto.

Alisema, mshindi wa uchaguzi huo William Ruto alifanikiwa kupita kikwazo cha kura asilimia 51 ya kikatiba, huku akiongeza kwamba mbinu iliotumika na tume ya uchaguzi kupata asilimia 64.4 ya wapiga kura ilikuwa sahihi.

"Hakukuwa na ushahidi kwamba fomu za uchaguzi katika tovuti ya matokeo ya mtandaoni zilibadilishwa kutoka fomu za awali zilizochapishwa," alisema.

Agosti 15 mwaka huu, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ilimtangaza Ruto kuwa Rais mteule baada ya kupata kura milioni 7,176,141 sawa na asilimia 50.49, dhidi ya milioni 6,942,930 za Odinga, ambaye alipata asilimia 48.85.

Raila Odinga, aliwasilisha mahakamani malalamiko yake akidai kwamba kura hiyo ilibadilishwa ili kumpa mpinzani wake William Ruto ushindi mwembamba katika uchaguzi huo uliokuwa na ushindani mkali.

***RFI***




Wafuasi wa William Ruto wakisherehekea ushindi wake mjini Eldoret, baada ya Mahakama ya Juu nchini Kenya kuidhinisha uteuzi wake. **PICHA: MTANDAO**

# 10 wauawa kwa kuchomwa kisu Canada

**WELDON, CANADA**

POLISI nchini Canada wanaendelea na msako wa watu wawili wanaoshukiwa kuwauwa watu 10 na kuwajeruhi wengine 15 kwa visu, tukio linalotajwa kuwa baya kuwahi kutokea kwa siku za karibuni.

Kamishna msaidizi wa polisi wa Canada, Rhonda Blackmore, aliwaambia waandishi wa habari kwamba jeshi lake lilipokea simu kutoka eneo linalokaliwa na jamii za wenyeji karibu na mji wa Weldon jimbo la Saskatchewan Septemba 4 mwaka huu, wakitaarifiwa juu ya kutokea kwa tukio hilo.

Kamishna huyo alithibitisha pia kuwa watu wengine 15 waliojeruhiwa walikuwa wamepelekwa katika hospitali mbalimbali za eneo hilo.

"Tuna maeneo 13 ya uhalifu tunayoyachunguza, kwa hivyo katika baadhi ya maeneo hayo kunaweza kukawa hakuna mtu aliyeuawa, kunaweza kukawa na majeruhi ambao hawakuuawa, kwa sasa msisitizo wetu ni kuwakamata washukiwa na kuwaweka ndani ili kuhakikisha usalama wa umma," alisema.

Aliongeza kuwa, baadhi ya wahanga wa mauaji hayo ya kushitukiza walilengwa na washambuliaji lakini wengine walishambuliwa ovyo ovyo.

Aidha, ilibainishwa kuwa polisi hadi sasa haijajuwa dhamira ya mashambulizi hayo na wala kutoa undani wa washukiwa wenyewe, lakini vyombo vya habari tayari viliyataja majina ya washukiwa kuwa ni ndugu wawili, Myles na Damien Sanderson, wenye umri wa miaka 30 na 31, ambao polisi ilisema walikimbia na gari.

Pia, ilielezwa kuwa eneo la James Smith Cree Nation lenye wakazi 2,500 lilitangaza hali ya hatari, huku wakazi wengine wa jimbo la Saskatchewan wakitakiwa kusalia majumbani mwao.

Waziri Mkuu Justin Trudeau, aliyaita mashambulizi hayo kuwa ya kusikitisha, huku akitumia mtandao wa Twitter kutuma salamu za rambirambi na kuwataka raia kutii maagizo yanayotolewa na mamlaka zao wakati huu msako ukiendelea.

Taarifa ya DW ilieleza kuwa picha za televisheni zilionyesha nyumba chache katika maeneo ya mashambani katikati ya machaka ya majani na miti mirefu zikiwa zimezungushiwa utepe wa polisi, huku kwenye mitandao ya kijamii kukisambazwa picha za hali ilivyokuwa baada ya mashambulizi hayo.

Mmoja wa mashahidi wa tukio hilo, Diane Shier, aliliambia shirika la habari la Canada kwamba jirani yake aliyekuwa akiishi na mjukuu wake ni miongoni mwa waliouawa.

Katika miaka ya hivi karibuni, Canada imeshuhudia wimbi la mashambulizi ya watu silaha katika maeneo ya umma, jambo ambalo halikuwa likitajwa sana kwenye taifa hilo linalopakana na Marekani, iliyozowea mikasa ya aina hiyo.

Miongoni mwa matukio makubwa nchini Canada katika miaka ya karibuni ni ofisa mmoja wa polisi kuwauwa watu 22 katika mji wa Nova Scotia, mwengine aliyewauwa waumini sita na kuwajeruhi watano katika msikiti mmoja mjini Quebec na dereva aliyewaponda waenda kwa miguu na kuwauwa 11 akiwajeruhi wengine 16 mjini Toronto.

***DW***

# KINANA ATOA NENO UJENZI UWANJA WA KISASA GEITA

**Na Beatrice Shayo, Geita**

WAKATI awamu ya kwanza ya ujenzi wa uwanja mpya wa soka wa kisasa wa Magogo unaojengwa katika Halmashauri ya Geita, ukielekea hatua za mwisho huku ukitarajiwa kuchukua jumla ya watazamaji 30,000 pindi utakapokamilika rasmi, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, ameutaka uongozi wa halmashauri hiyo kuhakikisha unakuwa na viwango vya kimataifa. Uwanja huo unajengwa kwa ushirikiano wa Kampuni ya Mgodi wa Madini ya Dhahabu ya Geita (GGM), na Halmashauri ya Geita.

Akizungumza na gazeti hili juzi, Mkandarasi Mshauri wa ujenzi huo kutoka Chuo cha Ardhi (ABECC), Godfrey Nyaluke, alisema ujenzi wa uwanja huo upo vizuri katika awamu ya kwanza kwa kufanya maboresho na awali walipanga jukwaa la VIP kuchukua watu 15,000, lakini kwa sasa litakuwa la watu 550 kwa kuzingatia vigezo vya usalama kwa kuongeza ghorofa moja na eneo la chini litabeba watu 400.

Alisema, ujenzi wa awamu ya pili utahusisha majukwaa ya watazamaji yatakayozunguka uwanja mzima ili kuwezesha watu 30,000 kuingia na kuufanya uwanja huo kuwa bora kati ya vitatu vilivyopo hapa nchini.

Nyaluke, alitoa kauli hiyo baada ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Kinana, kuutaka uongozi wa Mkoa wa Geita, kufuatilia kwa makini ujenzi wa uwanja huo, kwa kuhakikisha unakuwa na viwango vya kimataifa ili kutimiza dhamira ya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kufanikisha Fainali za Mataifa ya Afrika kufanyika nchini.

Kinana alitoa rai hiyo juzi baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa uwanja huo ambao awamu ya kwanza inaelekea kukamilika.

Aliwataka viongozi wa mkoa huo kwa kushirikiana na Kampuni ya GGM, kuhakikisha uwanja huo unakamilika kwa wakati na ifikapo mwaka 2027, uwe umekidhi vigezo vinavyotakiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika, CAF.

"Niwapongeze GGM kwa ujenzi wa uwanja huu mzuri wa kisasa, wamejitahidi kuumaliza kwa wakati kwa sababu ni uwanja muhimu kwa Mkoa wa Geita. Niwaarifu, nadhani wiki mbili au moja iliyopita, kulikuwa na mkutano wa CAF jijini Arusha," alisema Kinana na kuongeza;

"Rais Samia ana dhamira ya kuleta mashindano ya Kombe la Afrika mwaka 2027 nchini Tanzania, ndugu zangu wa Geita nimewasikia mkisema lengo lenu ni kuweka 'steji' za kukaa watu, mkifanya hivyo mtakuwa mmemaliza na tunafahamu miundombinu ya michezo ina umuhimu wake."

Aidha, Kinana alisema Tanzania inafikiriwa kwenye michuano mikubwa ya kimataifa na kwamba haimanishi inapendelewa, bali lazima wahakikishe wanakidhi vigezo kuanzia sasa mpaka ifikapo mwaka 2027.

**MAJESHI...**




Baadhi ya wanariadha wa majeshi kutoka nchi za Afrika, wakitimua mbio za mita 400 jana, katika mashindano yanayoendelea kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Meridianbet yaimwagia mamilioni KMC FC

**Shufaa Lyimo na Hadija Mngwai**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri Matokeo Tanzania ya Meridianbet, imeingia mkataba wa miaka mitatu wa kuidhamini timu ya Manispaa ya Kinondoni (KMC FC), wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200.

Akizungumzia mkataba huo wakati wa kuusaini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya KMC, Songoro Mnyonge, alisema amefurahi kusaini mkataba huo na kuahidi kushirikiana bega kwa bega na Meridianbet katika kuutekeleza.

"Tumefurahi Kampuni ya Meridianbet kuwa mdhamini wetu mkuu, tunaahidi kushirikiana nayo kwa lengo la kuifikisha mbali timu yetu.

"Mkataba tulioingia nao ni mnono zaidi ya NBC ambao wanatupatia milioni 10 kwa mwezi, hawa (Meridianbet) wanatulipa mara mbili ya pesa hizo," alisema Mnyonge.

Mwenyekiti huyo, alisema ujio huo wa Meridianbet, umekuja wakati muafaka kwani utalipa nguvu benchi lao la ufundi pamoja na kuongeza ari kwa wachezaji wao kujituma zaidi.

Aidha, alisema ujenzi wa uwanja wao uliopo Mwenge unaendelea vizuri na kwa sasa upo hatua za mwisho na kwamba msimu ujao wataanza kuutumia.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Kampuni ya Meridianbet, Cheta Chudasama, alisema ni mara ya kwanza kwao kudhamini timu inayoshiriki Ligi Kuu.

"Ni mara ya kwanza kudhamini timu inayoshiriki Ligi Kuu, hatutaishia hapa, tutaendelea kuzidhamini timu nyingine,

"Tumeamua kuidhamini KMC kwa sababu imekuwa ikifanya vizuri kwenye ligi na ni miongoni mwa timu zenye wachezaji bora," alisema Chudasama

## Kocha mpya Azam sasa kimeeleweka

**Na Adam Fungamwango**

KITENDAWILI cha nani atarithi mikoba ya Abdihamid Moallin katika jukumu la kuinoa Azam FC, kinatarajiwa kuteguliwa rasmi mwishoni mwa wiki hii, imeelezwa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', amesema mpaka kufikia jana kwenye meza ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Abdulkarim Amin 'Popat' kuna wasifu wa makocha unaokaribia 400 ambao hata hivyo wote ni wa kigeni.

"Wasifu unakaribia 400 sasa, kwenye meza ya Ofisa Mtendaji Mkuu wetu, lakini kwa bahati mbaya kama ilivyokuwa wiki iliyopita hakuna kocha yeyote mzawa ambaye ametuma maombi ya kutaka kazi ya kukinoa kikosi, lakini mchakato unaendelea, tunaendelea kuchuja majina na mpaka sasa tumefikia pazuri.

"Naweza kusema hadi mwishoni mwa wiki hii tutakuwa tumemtangaza kocha mpya, na kama bado hatujamtangaza, basi tutafanya hivyo Jumatatu, lakini atakuwa tayari ameshapatikana," alisema Zaka Zakazi.

## Kilimani City yapania kubeba 3 za Mundu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kilimani City, imesema inatarajia kuuanza vizuri msimu huu ili kutimiza malengo yake ya kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

Kilimani City, inatarajia kutupa karata yake ya kwanza Ligi Daraja la kwanza Kanda ya Unguja inayoanza kutimua vumbi leo kwa kuvaana na Mundu FC ya Nungwi, kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Tazari Mkoa wa Kaskazini majira ya saa 10 alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kilimani City, Omar Khamis Matu, alisema amekiandaa kikosi chake msimu huu kuwa cha ushindi zaidi ili kuweza kupanda daraja.

Alisema, malengo yake makubwa ndani ya timu hiyo ambayo kwa mara ya kwanza kikosi hicho kipo chini yake, ni kuhakikisha inafanya vizuri katika michezo yote ya mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo.

"Katika mchezo wa kwanza kila timu inahitaji kupata matokeo mazuri ili kuwapa moyo mashabiki wao, pia hata wachezaji kuongeza hamasa na kujituma, na sisi tumejiandaa kupata alama tatu katika mchezo huu," alisema.

## ZISIKUPITE

### KANE ASHAURIWA SPURS

HARRY Kane ameambiwa akatae kusaini mkataba mpya Tottenham Hotspur, huku Bayern Munich wakimtaka mshambuliaji huyo wa England mwenye miaka 29. ***(Bild, via Sun)***

### GALLAGHER AWANIWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace itapeleka ofa ya pauni milioni 20 kwa ajili ya kiungo wa Chelsea na England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 22, Januari baada ya kufanya vema pale Selhurst Park msimu uliopita alipokuwa anacheza kwa mkopo. ***(Mail)***

### UNITED YAWEKWA SOKONI

FAMILIA ya Glazer imeweka bei ya pauni bilioni 3.75 kwa timu yao ya Manchester United, na hilo linaweza kuwavutia wanunuzi kutoka Dubai. ***(Mail)***

### TAVARES ATAKA KUUZWA

MLINZI wa Arsenal na timu ya Taifa ya Ureno, Nuno Tavares mwenye umri wa miaka 22, amesema alitaka awekewe kipengele cha kununuliwa kwenye mkataba wake wa mkopo wa Marseille. ***(RMC Sport, via Mirror)***

### TIELEMANS NA ARSENAL

ARSENAL haikukaribia kumsajili kiungo wa Leicester mwenye umri wa miaka 25, Youri Tielemans licha ya kuhusishwa na uhamisho huo wa pauni milioni 25. ***(CaughtOffside)***

### GAVI AWANIWA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inamtaka kinda wa miaka 18 wa Barcelona na Hispania, Gavi, ambaye mkataba wake unamalizika msimu ujao. ***(Christian Falk)***

### GAKPO AWINDWA LEEDS

KLABU ya Leeds United itajaribu tena kumsajili mshambuliaji wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23 Januari, baada ya kushindwa kumsajili dirisha la sasa la majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### JUVE KWA FIRMINO

KLABU ya Juventus inatarajiwa kupeleka ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Liverpool na Brazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 30 Januari. ***(Liverpool Echo)***

### SOYUNCU NA GALATASARAY

KLABU ya Galatasaray inataka kumsajili mlinzi wa Uturuki, Caglar Soyuncu mwenye umri wa miaka 26, kabla ya kufungwa kwa dirisha lao la usajili wiki ijayo baada ya kuwekwa nje ya kikosi cha Leicester kilichocheza na Brighton Jumapili. ***(Leicestershire Live)***


### CHELSEA MKURUGENZI BADO

KLABU ya Chelsea bado haijampata mkurugenzi wa michezo huku mlinzi wa zamani wa Barcelona, Maxwell na mwingine wa Liverpool, Michael Edwards wakiwa kwenye orodha ya wanaowania nafasi hiyo. ***(Express)***

### MOURA KUMALIZA MKATABA

LUCAS Moura yuko tayari kumalizia mkataba wake na kuondoka Tottenham Hotspur, kama mchezaji huru mwaka 2024 baada ya ofa zilizokuja siku ya mwisho wa usajili kutoka Newcastle na Aston Villa kwa ajili ya winga huyo Mbrazil mwenye miaka 30 kukataliwa. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ANTONY AAHIDI MABAO MENGI ZAIDI MAN UNITED

●●● Mapenzi yangu yote kwa mapokezi haya, twende zaidi huo ni mwanzo tu...

**MANCHESTER, England**

BAADA ya mchezo wake wa kwanza wa Manchester United, Antony amesema ni ishara ya mambo yajayo kutokana na kufunga bao katika ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Arsenal, Jumapili.

Winga huyo wa zamani wa Ajax, aliyesajiliwa kwa dau la awali la pauni milioni 81.3 katika dirisha lililofungwa Alhamisi, amekuwa Mbrazil wa 100 kucheza katika Ligi Kuu England.

Alianza kucheza kwa saa moja kabla ya nafasi yake kuchukuliwa na Cristiano Ronaldo, ikiwa ni mechi yake ya kwanza kwa 'Mashetani Wekundu' na alifunga bao dakika ya 35.

Arsenal, walisawazisha dakika chache baada ya kuondoka kwake kupitia kwa Bukayo Saka, lakini Marcus Rashford, alifunga mara mbili na kufanya matokeo kuwa 3-1.

Akiwa na umri wa miaka 22 na siku 192, Antony alikuwa Mbrazil mwenye umri mdogo zaidi kufunga bao kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England.

Baada ya mchezo huo, Antony aliandika kwenye Twitter: "Siku ya ajabu kama nini! Shukrani kubwa kwa wafanyakazi wote wa MU na wachezaji wenzangu!! Sitasahau siku hii!

"Kwa mashabiki wa United, mapenzi yangu yote kwa mapokezi haya! Twende zaidi! Huo ni mwanzo tu!"

Naye nahodha wa zamani wa United, Roy Keane anaamini Erik ten Hag amefanya maajabu kubadilisha timu iliyofungwa 2-1 na Brighton and Hove Albion na 4-0 na Brentford katika michezo yao miwili ya ufunguzi wa msimu.

"Ana kundi la wachezaji anaofurahishwa nao na anaweza kufanya nao kazi," alisema Keane akinukuliwa na Sky Sports.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
AZAM
1 | 1.54
X | 3.43
2 | 6.28

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO ALIA NA BAHATI AS ROMA



**ROME, Italia**

JOSE Mourinho, amedai AS Roma hawakuwa na bahati baada ya kuchezea kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa Udinese, akisisitiza Paulo Dybala alikuwa mchezaji bora zaidi uwanjani.

Mabao kutoka kwa Destiny Udogie, Lazar Samardzic, Roberto Pereyra na Sandi Lovric yaliiacha Roma ikipoteza kwao kwa mara ya kwanza kwenye msimu huu, Jumapili huku Mourinho akipata kipigo chake kikubwa zaidi kwenye mechi za Serie A.

Ni mara moja tu katika maisha yake ya ukocha ambapo Mourinho alikumbana na kipigo kikubwa zaidi katika mechi ya ligi ya ndani, wakati alipofungwa 5-0 na Barcelona ya Pep Guardiola alipokuwa kocha wa Real Madrid mwaka 2010.

Licha ya kufungwa, Roma walimiliki sehemu kubwa zaidi ya mpira (asilimia 56.9) na kurekodi mikwaju mingi (12 hadi 11) kuliko wenyeji wao na Mourinho anaamini makosa ya safu ya ulinzi yaliwagharimu 'Giallorossi' hao.

"Leo (juzi) tulikuwa na bahati mbaya, tulitoa mabao mawili ambayo yaliamua mechi," alisema.

"Nazungumzia bahati mbaya kwa sababu mwanzoni tulikuwa tunaenda kwa nguvu kutokana na nafasi aliyoitengeneza Dybala, ambaye kwangu alikuwa mchezaji bora zaidi uwanjani.

"Ni wazi kwamba baada ya kupoteza kwa mabao 4-0, mtu anaweza kucheka, lakini alitoa ubora mkubwa.

"Niliwaambia wachezaji kwamba Udinese inaposonga mbele ni wazuri kwa kila kitu, ni wazuri katika kujilinda na kushambulia, huku sisi tukiwa hatuna mwisho bora."

# Giroud kufuata nyayo za Ibrahimovic

**MILAN, Italia**

OLIVIER Giroud anatumaini kufuata nyayo za Zlatan Ibrahimovic kwa kucheza kwa miaka mingi, huku akilenga kujumuishwa katika kikosi cha Ufaransa cha Didier Deschamps kwa ajili ya Kombe la Dunia nchini Qatar.

Giroud alifunga bao wakati AC Milan ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya wapinzani wao, Inter, Jumamosi, likiwa bao lake la 13 katika mechi 25 tu za Serie A alizoanza akiwa na 'Rossoneri' hao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, alisaini mkataba wa awali wa miaka miwili alipohamia Italia Julai 2021, lakini anatamani kucheza hadi mwisho wa msimu huu na ametiwa moyo na njaa ya mshambuliaji mwenzake wa Milan, Ibrahimovic.



Akizungumza na Telefoot, Giroud alisema: "Bado nina ari na dhamira. Nadhani hali ya akili ni muhimu katika umri wangu.

"Ningependa kuendelea, lakini ikiwa tu mwili wangu utaniruhusu.

"Nilikuwa najadiliana na Ibra. Kwake ni hivyo hivyo, Zlatan bado ana njaa."

Ibrahimovic, mwenye umri wa miaka 40, alifunga mara nane Milan ilipomaliza kusubiri kwa miaka 11 kutwaa taji la Scudetto msimu uliopita.

Wakati ushindi wa Scudetto wa Milan uliwakilisha taji la kwanza la ligi kwa Giroud tangu kushinda Ligue 1 na Montpellier msimu wa 2011-12, pia alibeba Kombe la Dunia mwaka 2018 akiwa na Ufaransa.

Giroud, ambaye amebakiwa na mabao matatu tu kumfikia Thierry Henry, kama mchezaji aliyeifungia mabao mengi zaidi timu ya taifa, anatamani kushiriki kombe lake la tatu la dunia baadaye mwaka huu.

"Sijui chochote kwa sababu mimi si kocha. Lakini ni wazi lazima niwe na lengo la kucheza Kombe la Dunia," alisema.

"Kwa historia yangu na Ufaransa, kuwa na nafasi ya kucheza Kombe la Dunia la tatu ni nafasi."

Y | CHEZA USHINDE KASINO

# BARRICK NORTH MARA YAJA NA KOMBE LA MAHUSIANO TARIME

**Na Mwandishi Wetu**

MGODI wa Dhahabu wa Barrick North Mara, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tarime, umeandaa mashindano ya soka ya kuwania Kombe la Mahusiano (Mahusiano Cup), yatakayojumuisha vijiji 16 vinavyozunguka mgodi huo.

Mashindano haya yenye kaulimbiu ya 'Mahusiano Bora kwa Uwekezaji Endelevu', yalizinduliwa rasmi jana katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Ingwe wilayani Tarime huku uzinduzi huo ukihudhuriwa na wananchi kutoka vijiji mbalimbali pamoja na wafanyakazi wa Barrick North Mara.

Katika uzinduzi huo, ambao mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mtenjele, ambaye aliongozana na viongozi mbalimbali wa serikali wilayani humo, waliburudika kwa kushuhudia michezo mbalimbali ikiwamo ngoma za asili.

Akizungumzia mashindano hayo, Kanali Mntenjele, aliwataka washiriki kucheza kwa amani na wasimamizi husika kutenda haki bila kupendelea timu yoyote.

Kwa upande wa Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko, alisema michezo ni nyenzo muhimu katika kujenga na kudumisha uhusiano katika jamii, ndiyo maana wameona ipo haja ya kuandaa mashindano hayo.

"Bila mahusiano bora na jamii inayotuzunguka sisi kama kampuni, hatuwezi kufanya kazi kwa utulivu, hali ambayo inaweza kusababisha uwekezaji wetu usilete manufaa katika pande zote mbili,"alisema.

Naye Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, aliipongeza Barrick North Mara, kwa kuandaa mashindano hayo kwa kuwa yatahamasisha ushirikiano kutoka kwa jamii inayozunguka mgodi huo ili kuwezesha kila upande kunufaika.

Vijiji ambavyo timu zake zinashiriki mashindano hayo ni Genkuru, Msege, Komarera, Nyamwanga, Kewanja, Nyakunguru, Kerende, Nyabichume, Mji Kati, Matongo, Nyangoto, Mrito, Keisangoro na Nyarwana.



Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mntenjele (mbele), akizungumza na timu za Kewanja FC na Mosege FC wakati wa uzinduzi wa mashindano ya Mahusiano Cup wilayani humo juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Yanga Princess yapania kufuta ufalme Simba Queens

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema wanatengeneza timu bora itakayowaletea ushindani na kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara kwa kuzima ufalme wa Simba Queens ambao wametwaa taji hilo kwa misimu mitatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lema, alisema wamefanya usajili wa wachezaji bora ili kufikia malengo yanayotarajiwa na Wanayanga.

Alisema wamesajili wachezaji kulingana mahitaji ya timu na wamerudi uwanjani kufanyia kazi mbinu na kutengeneza timu itakayoleta ushindani mkubwa katika ligi.

"Tunaweza kusajili wachezaji bora na usiwe na timu bora itakayoleta ushindani mkubwa, kazi kubwa kwa sasa ni kuandaa kikosi chetu kwa ajili ya kupambana kupata matokeo chanya, si kuwafunga watani wetu (Simba Queens)," alisema Lema.

Kocha huyo alisema wanakuja kivingine, hivyo wanapambana kuandaa timu kwa ajili ya kufikia malengo yao kwa msimu huu kutwaa ubingwa wa Ligi ya Wanawake.

Alisema, wamefanya usajili mzuri kwa kuboresha kikosi cha timu hiyo baada ya kuondokewa na baadhi ya wachezaji.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 06/09/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3421 | Jeju Utd vs Incheon Utd | 1.92 | 3.34 | 3.59 |
| 13:00 | 3511 | Zwiegen Kanazawa vs V Varen Nagasaki | 3.82 | 3.23 | 1.89 |
| 13:00 | 3835 | CS Maritimo U23 vs SP. Braga U23 | 3.34 | 3.49 | 1.95 |
| 13:30 | 3035 | Suwon City vs Pohang Steelers | 3.29 | 3.39 | 1.99 |
| 13:30 | 4116 | Gangwon vs Sangju Sangmu | 2.04 | 3.33 | 3.23 |
| 14:30 | 1585 | Beijing Guoan vs Hangzhou NG | 2.80 | 3.24 | 2.31 |
| 15:00 | 1151 | Coventry U23 vs Millwall U23 | 1.60 | 4.12 | 4.32 |
| 15:00 | 5151 | Kongsvinger 2 vs Molde FK 2 | 7.40 | 6.00 | 1.28 |
| 15:30 | 4322 | FC Samgurali Tskaltubo vs Dinamo Batumi | 5.20 | 3.50 | 1.67 |
| 15:45 | 5147 | FC Gagra vs Torpedo Kutaisi | 2.15 | 3.20 | 3.10 |
| 16:00 | 2619 | Gasogi United vs Etincelles | 2.04 | 2.99 | 3.63 |
| 16:00 | 3509 | Musanze vs Marines FC Gisenyi | 2.16 | 2.89 | 3.43 |
| 16:00 | 4314 | Geita Gold FC vs Kagera Sugar | 2.21 | 2.71 | 3.59 |
| 17:00 | 1532 | Ittihad AL Ramtha vs Al-Yarmouk | 1.89 | 3.20 | 3.88 |
| 17:30 | 3639 | Esteghlal Tehran vs Peykan FC | 1.44 | 3.78 | 7.06 |
| 18:00 | 1136 | FK Panevezys B vs FK Ekranas | 3.73 | 4.12 | 1.70 |
| 18:00 | 4474 | Oureskolernes BK vs Hobro | 5.88 | 4.61 | 1.40 |
| 18:15 | 5555 | Atlantis FC vs Lahden Reipas | 2.46 | 3.74 | 2.35 |
| 18:30 | 1371 | USM Alger vs JS Kabylie | 1.91 | 2.81 | 4.53 |
| 18:30 | 4277 | CR Belouizdad vs MC Oran | 1.34 | 4.50 | 8.60 |
| 19:00 | 1706 | Young Africans vs Azam | 1.54 | 3.43 | 6.28 |
| 19:00 | 1759 | Santos Laguna U20 vs Necaxa U20 | 1.95 | 3.50 | 3.55 |
| 19:00 | 5216 | Sarpsborg Sparta 2 vs Fredrikstad FK 2 | 2.11 | 4.60 | 2.55 |
| 19:45 | 3083 | Borussia Dortmund vs Copenhagen | 1.32 | 5.39 | 7.39 |
| 19:45 | 3498 | Dinamo Zagreb vs Chelsea | 6.22 | 4.31 | 1.45 |
| 20:00 | 3289 | Jonkopings Sodra vs Osters IF | 3.82 | 3.62 | 1.92 |
| 20:00 | 3519 | Trelleborgs FF vs AFC Eskilstuna | 1.72 | 3.98 | 4.38 |
| 20:00 | 5936 | Hammarby Talang FF vs Sollentuna Utd FF | 2.25 | 3.50 | 2.71 |
| 20:20 | 1395 | Al-Sailiya SC vs Al Arabi Doha SC | 4.42 | 3.83 | 1.63 |
| 20:20 | 4578 | Al Gharafa SC vs Umm-Salal SC | 2.07 | 3.43 | 3.08 |
| 20:30 | 3282 | Cape Town City vs Sekhukhune United | 2.09 | 2.94 | 3.83 |
| 21:00 | 2275 | Deportivo Espanol W vs Ferro Carril Oeste | 10.00 | 9.40 | 1.15 |
| 21:45 | 2235 | Colchester vs Brighton U23 | 2.23 | 3.48 | 2.74 |
| 21:45 | 2380 | South Shields vs Guiseley | 2.13 | 3.33 | 3.04 |
| 21:45 | 3038 | Liversedge vs Atherton Collieries | 2.28 | 3.25 | 3.00 |
| 21:45 | 5177 | Matlock Town vs Stafford Rangers | 1.95 | 3.45 | 3.55 |
| 21:45 | 5213 | Forest Green vs Accrington | 2.20 | 3.44 | 2.99 |
| 21:45 | 5409 | Bamber Bridge vs Marine FC | 1.95 | 3.50 | 3.50 |
| 21:45 | 5602 | Hyde United FC vs Utd of Manchester | 3.49 | 3.45 | 1.91 |
| 22:00 | 1582 | Paris St Germain vs Juventus | 1.37 | 4.83 | 7.06 |
| 22:00 | 2855 | Celtic vs Real Madrid | 5.00 | 4.10 | 1.57 |
| 22:00 | 2937 | RB Leipzig vs Shakhtar Donetsk | 1.20 | 6.40 | 11.01 |
| 22:00 | 3802 | Benfica vs Maccabi Haifa | 1.21 | 6.19 | 10.99 |
| 22:00 | 4375 | RB Salzburg vs AC Milan | 3.31 | 3.36 | 2.08 |
| 22:00 | 4563 | Sevilla FC vs Manchester City | 6.53 | 4.39 | 1.43 |
| 00:00 | 2334 | Envigado FC vs Rionegro Aguilas | 2.65 | 2.84 | 2.70 |
| 01:05 | 3833 | Leones Negros Udg vs Cancun FC | 1.98 | 3.24 | 3.48 |
| 03:00 | 1053 | Club Leon vs Juarez FC | 2.03 | 3.36 | 3.51 |
| 03:05 | 4600 | Santos Laguna vs Club Necaxa | 1.86 | 3.46 | 4.01 |
| 03:30 | 3367 | Palmeiras vs Atletico Pr | 1.39 | 4.22 | 6.87 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Septemba 6, 2022
Nipashe



## Antony aahidi mabao mengi zaidi United

# Yanga na Kisinda sasa kimeumana

## •••TFF yatoa sababu usajili wake kukwama, Nabi atema cheche akionya...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Shirikisho la Soka nchini (TFF), likizitaka Klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara hasusan zinazoshiriki michuano ya kimataifa kuzingatia kanuni za usajili wa wachezaji wa nje kuwa 12 kama kanuni inavyoeleza, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewaonya nyota wake.

Yanga ambayo itashuka dimbani leo kuikaribisha Azam FC kwenye mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa moja usiku, imekwama kufanikisha usajili wa nyota wa kigeni, Tuisila Kisinda, dakika za mwisho kabla ya dirisha la usajili Tanzania Bara kufungwa Jumatano iliyopita saa sita usiku.

Ingawa TFF, haikuitaja wazi klabu ambayo ilitaka kuongeza idadi ya wachezaji wa kigeni, lakini taarifa za ndani zilizolifikia gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya shirikisho hilo ni kwamba mabingwa watetezi hao wa Ligi Kuu, walitaka kuchomoa jina moja la wachezaji ambao tayari wameshapata leseni ya kushiriki Ligi ya Mabingwa kutoka CAF ili kumwingiza Kisinda na walipokwama wakataka idadi ya nyota wa kigeni waongezwe kuwa 13.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari na Mawasiliano ya TFF, Clifford Ndimbo, alisema usajili wa wachezaji wa kigeni kwa klabu zinazocheza mashindano ya kimataifa ulishapitishwa na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF.

Alisema kamati hiyo kupitia kanuni na taratibu tayari walikuwa na orodha ya usajili wa wachezaji ambao wamewasilishwa TFF na kupata leseni na tayari majina hayo yenye leseni yaliwasilishwa CAF na kupata leseni za CAF kuendana na muda.

"Wachezaji wote wa klabu hizo za Azam FC, Geita Gold, Simba na Yanga walishapewa leseni zao mapema kwa ajili ya msimu wa 2022/23, unaotumika kuwaombea usajili wa mashindano ya CAF, " alisema Ndimbo.

Majina ya nyota wa kigeni 12 ambayo Yanga iliwasilisha kwa ajili ya kuombewa leseni CAF ni Djigui Diarra, Djuma Shaban, Joyce Lumalisa, Yannick Bangala, Gael Bigirimana, Khalid Aucho, Jesus Moloko, Bernard Morrison, Lazarous Kambole, Fiston Mayele, Heritier Makambo na Stephan Aziz Ki.

Hata hivyo, wakati hayo yakiendelea, Kocha Nabi amewataka wachezaji wake kuelekeza akili zao kwenye mechi zilizopo mbele yao kwa kupambana mwanzo mwisho na kutokubali kulewa sifa.

Akizungumza na waandishi wetu, Nabi jana aliumulika zaidi mchezo wa leo dhidi ya Azam FC, na kusema hiyo ni dabi ya pili baada ya ile waliyoicheza na timu ya Simba kwenye Ngao ya Jamii.

Alisema ni mchezo ambao utakuwa mgumu na wa ushindani kwa kuwa timu zote zina uwezo mzuri na kudai mpinzani wao huyo mchezo uliopita alitoka sare na timu ya Geita jambo ambalo watahitaji pointi tatu, lakini pia wana kocha mpya ambaye anataka kuonyesha ubora wake.

"Hiyo ni dabi ya pili kwa upande wangu baada ya ile ya Simba, naiheshimu Azam, ina wachezaji wazuri tofauti na ya miaka minne iliyopita," alisema kocha huyo.

***Imeandaliwa na Shufaa Lyimo, Hadija Mngwai na Saada Akida***

**WAYAAA...**



Mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford, akiifungia timu yake moja kati ya mabao mawili aliyofunga wakati wakishinda 3-1 dhidi ya Arsenal kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi huku beki wa 'The Gunners', Ben White akijaribu kuzuia bila mafanikio. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yatangaza operesheni 3 kali

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza kaulimbiu mpya ya operesheni Septemba, ili kutekeleza mambo matatu ambayo wanatarajia kuyafanya mwezi huu, ikicheza mechi tatu za Ligi Kuu na mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema wana mambo makubwa matatu ambayo watatakiwa kuyatekeleza kwa usahihi, hivyo wamekuja na kaulimbiu hiyo.

"Mwezi huu tuna kitu kinaitwa 'Operesheni Septemba', ambapo tunataka kutekeleza mambo matatu kwa usahihi, kwanza ni kushinda mechi yetu ya Jumatano (kesho) dhidi ya KMC FC, kwa sababu tukifanya hivyo tutakuwa tumevuna pointi tatu na kufikisha tisa ambazo tulikuwa tunazihitaji kabla ya kwenda kucheza mechi za kimataifa.

Pili tuna operesheni nyingine ya kwenda kushinda mechi zetu Nyanda za Juu Kusini kwa sababu msimu uliopita hatukupata pointi yoyote dhidi ya timu za huko tukiwa Mbeya dhidi ya Prisons na Mbeya City, na ya tatu ni operesheni ya kwenda kushinda Malawi dhidi ya Nyasa Big Bullets, Septemba 10 na ya marudiano terehe 17. Mambo haya yote matatu makubwa mwezi huu, tumeamua kuja na kitu kinaitwa Operesheni Septemba kwani mechi hizo zote tano tutazicheza ndani ya mwezi huu," alisema Ahmed.

Baada ya mechi ya kesho ya Ligi Kuu dhidi ya KMC, Simba itakwenda kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa nchini Malawi na Septemba 14 itacheza dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, kabla ya kurudiana na Nyasa Big Bullets Septemba 17 na tarehe 28 mwezi huu itacheza dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kikosi cha timu hiyo kiliingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa na mechi hizo, huku klabu hiyo ikimwita pia beki wake wa kati Joash Onyango anayedaiwa hana furaha kutokana na kutokuwa kwenye kikosi cha kwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >